SUPA JACKPOT
TZS. 1,090,583,531
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MIAKA 2 YA SAMIA**
Sekta binafsi yazidi kustawi, kuongeza ajira




UKURASA 11

Jumatano Machi 15, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581250
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## Bandari jumuishi kupaisha uchumi visiwani Zanzibar

UKURASA 2



Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga

# Kilio wananchi masharti mapya bima ya NHIF

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Mkaguzi wa Polisi, Dumu Mwarugenge (kushoto), makao makuu ya Kikosi cha Usalama Barabarani, kuhusu baadhi ya ajali zinazosababishwa na makosa ya uzembe wa waendesha vyombo vya moto, wakati wa maonyesho ya maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani 2023, yaliyofanyika kitaifa jijini Mwanza jana. Wa pili kulia ni Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Wachambuzi wanavyoiona bajeti ya mwaka 2023/24

UKURASA 4

SPECIAL SUPPLEMENT ON COMPLETION OF TWO YEARS UNDER THE ABLE LEADERSHIP OF



HER EXCELLENCY DR. SAMIA SULUHU HASSAN

The Guardian Limited will publish a special supplement with **"The Guardian"** and **"Nipashe"** Newspapers, with a special report focusing on the achievements of the Government under the leadership of President **Dr. Samia Suluhu Hassan**

20th March 2023

We wish to invite you to be a part of this special supplement by publishing your **Special features, Congratulatory messages, Advertorials** and **Advertisements.**

The Guardian Nipashe

TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

617309101

MICHEZO SIMBA WAUNGANA KUIUA HOROYA AC UK. 24
KATUNI UK. 6

# Kilio masharti mapya bima NHIF

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), wameiomba serikali kuangalia upya uamuzi wake, maboresho sekta ya afya nchini yazingatie kundi maalumu kwenye jamii hususan watoto.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, alisema utafiti unaonesha kuna ongezeko la kipato sekta isiyo rasmi baada ya serikali kurasimisha maeneo mengi na Watanzania kuwa na uwezo wa kumudu gharama za bima.

"Kinachogomba ni kutotoa kipaumbele kwenye afya tutaendelea kutoa elimu kwa wale wasio na uwezo serikali haijawaacha nyuma wao watatibiwa kwa msamaha ilimradi taratibu za kumtambua amekidhi, lakini sio una smart phone una uwezo wa kununua bando la Sh. 2,000 useme huna uwezo, tumeona Watanzania wana uwezo na watamudu bima ya afya," alisema Konga.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi walisema hatua ya mfuko huo, wa utaratibu wa malipo ya Sh. 50,400 ya Toto Afya Kadi, umeondolewa kuanzia Machi 13, mwaka huu, kwa ambao bima zao zimekwisha na wanaohitaji kujiunga, ulihitaji maandalizi.

Baadhi yao wakitoa maoni yao kwa njia ya mtandao; Latifa Idd, mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, alisema amejiunga na mfuko huo mwaka 2018, kwa kumlipia mwanawe bima ya Sh. 50,400, kwa mwaka.

Alisema mwaka huo muda mfupi baada ya mwanawe kuanza kuhudumiwa na mfuko huo, aligundulika kuugua ugonjwa wa kifafa na kuhitajika kuhudhuria kliniki Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kila mwezi.

"Kumwona daktari bingwa kama nisingekuwa na bima ya afya gharama ni Sh. 30,000. Pia nilibaini dawa moja kati ya tatu ambazo anatumia mtoto wangu, inakupasa uwe na Sh. 45,000 na hapo bado dawa zingine mbili.

"Dawa nyingine moja inauzwa Sh. 25,000 ambayo ni vidonge 10 na inatakiwa ameze kwa siku 30, hivyo kwa mwezi ni Sh. 75,000 ya tatu gharama ni Sh. 36,000. Kwa hiyo utaona ningehitajika kuwa na zaidi ya laki moja kila mwezi, serikali itutazame kwa hili," alisema Latifa.

Alisema mabadiliko hayo watakaomudu ni ambao wana kipato rasmi, kuliko ambao hawajui kwa siku wataingiza kiasi gani cha fedha kutokana na shuguli zao za kila siku.

Fred Nashon, mkazi wa Tabata, Dar es Salaam, alisema mabadiliko hayo ingawa yanaweza kuwa na manufaa, mfuko ungeongeza gharama za malipo ya kifurushi hicho.

"Bora wangetuambia tulipie hata Sh. 70,000 hadi 100,000 kwa mwaka tungetafuta wazazi kuliko kusema watoto wajisajili kupitia shule, kaya au familia. Kwani shuleni huko ni wazazi wangapi wanataka kujiunga, walishindwa kulipia Sh. 50,400 kwa hiari, sembuse sasa," alisema Fred akiongeza.

"Dunia inapambana kupunguza vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano ikibidi kuondoa kabisa, sisi tunaondoa huduma muhimu ya afya kwa watoto, na vile vile serikali ikumbuke kwamba wananchi waliisaidia, sera inasema matibabu bure kwa mtoto, lakini bado mzazi akamkatia bima mtoto huyo huyo anayelindwa na sera."

Brigita Mwakatobe, mkazi wa Mbeya mjini, alisema mfuko huo ungeanza kufanya kampeni kwenye shule za msingi na sekondari, kwa kuwakutanisha wazazi na walimu ili kuhamasisha kundi kubwa la wanafunzi kujiunga na bima.

"NHIF kama ilivyosema wanafunzi, au shule zikipeleka idadi kubwa ya wanafunzi watawasajili kwa haraka. Lakini wazazi wengi elimu hii wanayo? Juzi tu, kikao cha shule kiliamua wanafunzi wa darasa la nne na la saba, wawe wanakula shuleni, kwa Sh. 15,000 kwa mwezi mwitiko ni mdogo," alisema.

Sally Mfalila, akitoa maoni kwenye mtandao wa twitter, alisema: "Kwa hili jamani hapana wanaumiza watu, watakaoteseka ni watoto, wangeweka maslahi yao nyuma, wangejua kiasi gani hii bima ilikuwa inatusaidia wazazi, hata ukitaka kumsaidia mtoto nwingine ilikuwa rahisi."

Suzan Magomba, kwenye ukurasa wa twitter, alisema kwamba: "Mimi nimelipia mwezi uliopita nategemea mwezi wa tano nipate kadi, leo tena inakuja hii, ina maana pesa yangu imekwenda bure? Nimelipia Sh. 50,400 kwa ajili ya ku-renew, uamuzi umekuja ghafla."

**NHIF YAFAFANUA**

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Konga alisema uzoefu wa miaka saba kuhudumia watoto kupitia utaratibu wa Toto Afya Kadi, umewafikia watoto 210,664 walio chini ya miaka 18.

Alisema kutokana na malalamiko yaliyokuwapo walilazimika kuja na maboresho ili kufikia kundi kubwa la watoto nchini, kwa kuzingatia sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 iliyoonyesha watoto chini ya miaka 18 ni asilimia 31 ya wananchi wote.

Kwa mujibu wa Konga, lengo la maboresho ya usajili wa watoto waliokuwa wanasajiliwa kupitia utaratibu huo ambao kwa sasa wazazi au walezi watawasajili kama wategemezi kwenye bima au kupitia shule wanazosoma ni kuongeza wigo wa wanachama kuelekea bima ya afya kwa wote.

"Mpango wa Toto Afya Kadi ulianza rasmi mwaka 2016 baada ya kufanyiwa upembuzi na lengo likiwa ni kuwajumuisha watoto kupitia shule zao. Kwa kipindi chote hiki mfuko umejifunza mengi na kati ya hayo ni usajili wa mtoto mmoja mmoja ambao unachelewesha utekelezaji wa dhana ya bima ya afya ambayo inataka watu kujiunga kwa wingi wao," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna sababu zingine ambazo hakuziweka wazi zilizosukuma maboresho hayo huku akisema utaratibu wa kusubiri kusajiliwa kwa siku 90 kabla ya kuanza kupata huduma, sasa kupitia utaratibu mpya watakaosajiliwa kupitia shule itachukua siku 30 na gharama kwa mwanafunzi mmoja ni Sh. 50,400.

Alisema wanachama wa Toto Afya ambao wapo kipindi cha kusubiri miezi mitatu kabla ya kuanza kupata huduma na wale ambao ni wanachama tayari kupitia utaratibu huo wataendelea kupata huduma hadi muda wa uanachama utakapoisha.

***Imeandikwa na Christina Mwakangale (DAR),**

# Bandari jumuishi kuchochea uchumi Zanzibar

**Na Jenifer Gilla**



Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Idara ya Itikadi na Uenezi, Khamisi Mbeto Khamisi (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Kiwanda cha Uchapaji cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Balasubramaniyan Venkachalam (kulia), alipotembelea ofisi za TGL, Mikocheni mkoani Dar es Salaam jana. Wengine ni Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (wa pili kulia) na Mhariri Mtendaji msaidizi wa gazeti hilo, Epson Luhwago. **PICHA: MIRAJI MSALA**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inajenga bandari jumuishi yenye ukubwa wa kilometa moja, ili kukuza uchumi wa nchi.

Bandari hiyo ikikamilika, itakuwa na uwezo wa kupokea meli 10 kubwa kwa wakati mmoja kutoka ndani na nje ya nchi zilizobeba bidhaa mbalimbali yakiwamo makontena.

Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis, alisema hayo alipofanya ziara katika ofisi za kampuni ya The guardian Limited, Mikocheni, Dar es Salaam.

Alisema bandari hiyo itakuwa pia na eneo la kuhifadhi mafuta, hivyo kusaidia kutimiza lengo la Zanzibar kuwa muuzaji mkubwa wa mafuta kwa kuwa sasa inatumia takribani lita milioni 15 kwa mwezi.

Kwa mujibu wa Khamis, tayari kampuni moja ya Bakresa imejenga bohari ya mafuta yenye ujazo wa hifadhi wa lita milioni 21 na kuhimiza kampuni zingine ziendelee kujenga. "Maana yake tunaelekea Zanzibar kuwa wauzaji wa mafuta ukizingatia ina mchakato wa kuchimba mafuta yake. Kwa hiyo tunajenga hiyo bandari ili pia kurahisisha mchakato wa biashara ya mafuta," alisema.

Pia alisema serikali ya Zanzibar kwa sasa inajenga uwanja wa ndege wa kimataifa wa Pemba utakaokuwa na uwezo wa kupokea ndege kubwa aina ya Boeing 737 yenye uwezo wa kuchukua takriban abiria 300 lengo likiwa ni kukuza uchumi wa visiwa hivyo.

Kiongozi huyo pia aliiomba jamii kuwapuuzia wote wanaolalamikia Muungano kuwa hauna maslahi kwa Zanzibar. Alisema matamko hayo si ya kweli kwa kuwa kila kinachoingia kwa jina la Muungano, Zanzibar inapata gawio lake kwa mujibu wa sheria.

"Kwa mfano hivi juzi tu umekuja msaada wa UVIKO -19 kutoka IMF (Shirika la Fedha la Kimataifa). Mama Samia (Rais Samia Suluhu Hassan) akaelekezwa kwa mujibu wa gawio Zanzibar inapata asilimia 4.5. haikuwa hisani ile, kikija chochote kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar ina sehemu yake kwa mujibu wa sheria," alisema.

Kuhusu maendeleo ya kiuchumi, alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa ndani ya miaka miwili uongozi wa Rais Dk. Husein Ali Mwinyi katika sekta za afya, elimu na miundombinu ambayo imechangia kukuza ustawi wa mwananchi na Zanzibar kwa ujumla.

Alisema Zanzibar kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imesajili miradi ya uwekezaji takribani 215 yenye thamani ya dola bilioni 306 huku pia kukiwa uwekezaji wa visiwa 16 vilivyogharimu dola milioni 3.26.

"Pia tunajenga barabara zenye urefu wa kilomita 275 kwa kiwango cha lami katika maeneo yote ya Zanzibar. Kati ya hizo kilomita 119 zinajengwa kwenye mkoa wa mjini tu. Serikali pia imeshajenga shule ghorofa tisa za kisasa kwa wanafunzi wa shule msingi, huku madarasa 811 yamejengwa," alifafanua.

aye Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, alimweleza Katibu huyo kuwa gazeti hilo linaunga mkono kazi nzuri zinazofanywa na serikali ya Zanzibar kwa kutenga ukurasa mzima kuandika habari kutoka visiwani humo, ili kuhabarisha umma mambo mazuri yanayoendelea huko.

# Sekta binafsi yazidi kustawi, kuongeza ajira

**Na Romana Mallya**



SEKTA binafsi ndio injini ya uchumi wa nchi duniani ikichangia ajira nyingi kupitia kampuni na viwanda katika kukabiliana na tatizo la ajira.

Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kuapishwa Machi 19, mwaka 2021, aliipa sekta hiyo kipaumbele kikubwa kwa kuhakikisha anashughulikia changamoto za mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji yaliyokuwa yakilalamikiwa ili itimize lengo lake.

Ndani ya miaka miwili ya Rais Samia, kwa nyakati tofauti amekutana na makundi mbalimbali wakiwamo wafanyabiashara na wawekezaji na kufanya ziara nchi mbalimbali duniani zenye lengo la kufungua milango ya uwekezaji.

Zipo juhudi zinazoifanya sekta binafsi kwa sasa kusherehekea mafanikio badala ya kuendelea kulalamikia.

Mwanzoni mwa mwezi Desemba mwaka 2022, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), iliandaa Siku ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSD22), kwa lengo la kusherehekea miaka miwili tangu Rais Samia aingie madarakani.

Sherehe hizo zilikwenda sambamba na kuainisha mafanikio iliyofikia likiwamo kitendo cha serikali kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji.

Mengine ni ongezeko la biashara Kenya kwa asilimia 95 kulikochangia ukuaji wa uchumi wa Tanzania na masoko mengine mapya duniani.

Ukweli wa mafanikio hayo ulidhihirishwa na hafla hiyo ambayo ilikutanisha wadau ambao ni wawekezaji wa ndani na nje ya nchi pamoja na wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo.

Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, ametaja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na ukuaji wa shughuli za uwekezaji, upanukaji wa wigo wa ajira, masuala ya kodi na bidhaa za Tanzania kufikia masoko mapya.

Hilo lilidhihirishwa na tuzo zilizotolewa siku hiyo kwa Kampuni na Vyama vya Biashara (PSOs) ambavyo vilionyesha utendaji wa kipekee kwa mwaka mzima.

Mafanikio hayo pia yalitaja juhudi mbalimbali zilizofanywa na Rais Samia katika kushughulikia janga la UVIKO-19 lililokumba dunia, zimewezesha kuwapo kwa ukuaji wa uchumi.

Sekta ya utalii ikiwa miongoni mwa mafanikio yaliyotajwa siku hiyo kwamba Rais Samia ameipaisha kupitia filamu ya The Royal Tour na katika kipindi cha miezi saba kilichoanzia mwezi Januari mwaka 2022, jumla ya watalii 742,133 walitembelea Tanzania.

Filamu hiyo imeongeza idadi ya watalii 285,867, sawa na asilimia 62.7 ikilinganishwa na mwaka uliopita (2021).

Mafanikio mengine yaliyotajwa ni ukuaji wa sekta ya kilimo uliotokana na mikopo nafuu kwa kitendo cha Rais Samia kutoa maelekezo, ikachangia riba za benki kupungua mfano CRDB ilishusha kutoka asilimia 20 mpaka asilimia tisa, NMB asilimia 10 mpaka asilimia tisa, TADB asilimia 11 mpaka asilimia tisa.

Kushuka kwa riba kumetajwa kuwa ni mafanikio kwa sekta binafsi na kufanya wadau wa kilimo kupata mikopo kwa unafuu na kukuza sekta ya kilimo sambamba na ajenda 10/30.

Mafanikio mengine ni kitendo cha nchi kuridhia mkataba wa kujiunga na Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) na kuifanya Tanzania kuchaguliwa kati ya nchi nane kuanza kuuza bidhaa zake katika eneo hilo kulikosababisha wanufaike na punguzo la kodi.

Hilo likaelezwa kuwa limefungua sekta hiyo ambayo inajiandaa kuwekeza kwenye viwanda ili wafanyabiashara wasafirishe mizigo yao nje ya nchi.

Sekta binafsi pia, imefurahishwa na kitendo cha Rais Samia kufungua masoko ya kimataifa na kuwezesha wafanyabiashara wa Tanzania kusafirisha parachichi kwenda nchi za Afrika Kusini, India na China pekee ikiagiza zaidi ya tani 40,000.

Mafanikio mengine ni kitendo cha serikali kudhibiti bei za mafuta kupanda kwa kutoa ruzuku kila mwezi na utiaji saini wa mikataba minne na kampuni za uchimbaji madini yenye thamani ya zaidi ya Dola milioni 735 uliofanyika mwaka 2021.

Eneo lingine ambalo Rais Samia ameligusa na kuifurahisha sekta binafsi ni ujenzi, baada ya kuondolewa kwa utaratibu wa serikali kufanya kazi za ujenzi wa miradi yake bila kutumia makandarasi (force account) na kuwasaidia kupata zabuni.

Upatikanaji wa vibali vya uwekezaji ni miongoni mwa maeneo yaliyokuwa yakilalamikiwa na baada ya Rais Samia kuingia madarakani alilishughulikia na sasa vinatolewa ndani ya muda mfupi.

Katibu Mkuu Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Abdallah Mwinyi, amefurahishwa na Rais Samia namna anavyoipa umuhimu sekta binafsi, baada ya kuingia madarakani alihakikisha kodi zinakuwa rafiki.

Anasema upo ushirikishwaji mkubwa baina ya sekta binafsi na umma huku akitolea mfano kika cha Februari 21 mwaka huu, kilichofanyika jijini Dodoma ambacho kimetoa fursa kwao kuwasilisha mapendekezo kuhusu uboreshaji wa sheria 24 za kodi.

"Tunaamini kwamba hali hii inavyoendelea kutakuwa na ufanisi mkubwa ndani ya sekta binafsi. Kwa hakika tuliyowasilisha yameyapokea vyema na hii inatupa moyo kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kufanya maboresho zaidi ya sheria za kodi, ili kuweka mazingira mazuri zaidi ya ufanyaji biashara na serikali ikakusanya kodi zake bila tatizo," anasema.

Anakumbushia baadhi ya mzigo iliyokuwa ikikamatwa na mamlaka husika ikitokana na sheria za kodi hasa za bandari kwa kuhusishwa na changamoto za risiti na baada ya mazungumzo anasema iliachiwa.

"Tunashukuru TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) ilielewa makosa yaliyojitokeza hasa ya wasimamizi wa sheria ya kodi na changamoto za kiforodha hivyo mizigo yote iliyokuwa imekamatwa waliiachia, haya ni mafanikio makubwa.

"Kuachiliwa huko kunaonyesha kuna shida mahali fulani, tulipokutana Februari 21, mwaka huu, jijini Dodoma, serikali imeonyesha kuelewa shida iliyopo na kukiri ipo kwenye viwango vya kodi.

"Tunaamini kamati tuliyokutana nayo itatoa ushauri mzuri serikalini ili viwango vya kodi vishuke na kuwa rafiki kwa wafanyabiashara," anasema.


## ANATAFUTWA



Familia ya Sentoke Ngendabanka wa Murukulazo wilaya ya Ngara inatangaza kupotelewa na ndugu yao Edwin Sentoke Ngendabanka mwenye umri wa miaka 70, aliyepotea tangu jumanne tarehe 8/3/2023 asubuhi.

Alikuwa amevaa fulana ya njano, suruali nyeusi, saa ya mkononi, yeboyebo nyeusi na alikuwa biblia mkononi.

Kwa sasa alikuwa anaishi Buhongwa Jijini Mwanza kwa Mchungaji Kajumla Israel Kuguru, wa kanisa la PEFA kata ya Iwanhima, mtaa Semba eneo la Sahwa juu wilaya ya Nyamagana.

Anatatizo la kupoteza kumbukumbu na hana uwezo wa kujieleza vizuri. Atakaye muona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu na kwa mawasiliano piga simu zifuatazo:

**0757680718 /0652471099 /0782832737 /0754664042 /0692032006 /0756709558. Taarifa ya Polisi: BHG/RB/612/23.**



## TANGAZO

### KATAZO LA SHUGHULI ZA KIBINADAMU NDANI YA HIFADHI YA MAKUTUPORA

Bodi ya Maji Bonde la Wami/ Ruvu imepewa jukumu la kusimamia rasilimali za maji ikiwemo Hifadhi ya Maji ya Makutupora kupitia Sheria Namba 8 ya Mwaka 2022.

Hifadhi ya maji ya Makutopora ina ukubwa wa Kilometa za Mraba 348.26km na ilishatangazwa kuwa hifadhi ya chanzo cha maji kupitia GN 202 ya mwaka 2002.

Hifadhi ya maji ya Makutopora ni chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 61,000 kwa siku na kunufaisha wakazi wapatao 564,229 kupitia Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira(DUWASA).

Kutokana na ongezeko la idadi ya watu na mahitaji ya Makazi kwenye jiji la Dodoma kumejitokeza uvamizi kwenye eneo la hifadhi ambapo wananchi wasio waaminifu wanauza viwanja na wengine kufanya shughuli za ufugaji na ukataji hovyo wa miti. Shughuli zote hizo zinaathiri wingi na ubora wa maji na kuhatarisha uhakika wa upatikanaji Maji safi na salama.

Rai inatolewa kwa wananchi wote kuacha mara moja shughuli hizo na kutonunua maeneo kwa maana ya viwanja na mashamba kwenye eneo hilo huku wakijiridhisha mipaka ya maeneo wanayouziwa jirani na hifadhi kwa kuwasiliana na Bodi ya Maji Bonde la Wami/ Ruvu na Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Dodoma kuepuka hasara na udanganyifu wowote.

Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Namba 8 ya Mwaka 2022 inasema kila mkazi aishiye Tanzania Bara ana wajibu wa kutunza, kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji ili viwe endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

***"TONE LA MAJI LAZMA LIHIFADHIWE"***

**Imetolewa na**
**Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu**
**Ofisi Ndogo Dodoma**
**P.O Box 456**
**Dodoma**
**Simu 0733779519/0714992367**

217322402

# Wachambuzi wanavyoiona bajeti 2023/24

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wametoa maoni juu ya sura ya bajeti ya mwaka 2023/24 ya kukusanya na kutumia Sh. trilioni 44.38 huku maeneo kipaumbele yakiwa ni kugharamia ajira za watumishi wapya wa sekta za afya na elimu, uchaguzi wa serikali za mitaa na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Bajeti hiyo imeongezeka kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na ya mwaka 2022/23 ya Sh. trilioni 41.48 na kujielekeza kwenye kugharamia miradi ya kielelezo inayoendelea, deni la serikali, mishahara ya watumishi wa umma, huduma za jamii zikiwamo afya, elimu, maji, kuimarisha misingi ya usawa mbele ya sheria.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Anna Henga, alisema kilichomfurahisha ni suala la watumishi wa serikali hasa ajira mpya ambazo zitakwenda kupunguza tatizo lililopo kwa sasa.

Anna alisema kuna changamoto ya ajira hasa vijana, kuongeza ajira mpya kutapunguza ombwe la vijana wengi waliomaliza shule na kutokuwa na kazi ambalo linaonekana kwenye taaluma nyingi nchini.

"Vijana wanahangaika kutafuta ajira imefikia mahali hadi madaktari nao wanakosa ajira, tunaposikia serikali inaweka kipaumbele cha kuajiri tena inatia moyo sana," alisema.

Alisema eneo jingine ni maslahi ya wafanyakazi kuongezwa ambayo yatasaidia kuongeza morali kwa kuwahudumia wananchi vizuri.

"Tunajua bajeti haiwezi kukidhi mahitaji yote kutokana na vyanzo tulivyonavyo ikilinganishwa na mahitaji, lakini inatia moyo unapoona inagusa maeneo muhimu," alisema.

Naye, Mhadhiri na Mtaalam wa Bishara na Uchumi wa Chuo cha Biashara CBE, Mariam Tabwe, alisema pamoja na kipaumbele cha ajira ni muhimu kuangalia elimu inayotolewa kwa kiasi gani inamwezesha mtu kujiajiri ili uwekezaji uliofanyika uwe na matokeo.

"Najua kwa sasa tupo kwenye mchakato wa mabadiliko ya mitaala yetu, naamini itakuwa yenye kumfanya mtu ajiajiri zaidi kuliko kusubiriwa kuajiriwa, kipaumbele hiki kiangaliwe kwa sura tofauti," alisema.

Alisema ni muhimu msukumo kwenye kilimo ukawekwa kwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo, na kila mwanadamu kwa kuwa chakula ni hitaji la lazima kwa nchi na dunia.

**VIPAUMBELE VINGINE**

Akiwasilisha mapendekezo ya serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/24 na Mfumo na ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka huo kwa wabunge juzi, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwingulu Nchemba, alisema mapendekezo ya ukomo huo yameongezeka ikilinganishwa na makadirio ya awali yaliyowasilishwa kwenye mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/24.

Aidha, serikali kwa mwaka huo itaweka msukumo katika kuimarisha sekta za uzalishaji ambazo zina fursa za kukuza uchumi, kuongeza mauzo nje, kupunguza utegemezi wa bidhaa toka nje na kuongeza mapato ya serikali.

Pia, kutekeleza diplomasia ya uchumi, kuimarisha mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na utekelezaji wa mkakati wa uchumi wa buluu.

Alisema hali hiyo inatokana na kumalizika kwa mazungumzo na Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika ambazo zimeahidi kutoa Sh. bilioni 1,166.9 na Sh. bilioni 247.4, mtawalia.

Alisema mfumo huo wa bajeti umezingatia makubaliano baina ya Serikali na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) chini ya programu ya Extended Credit Facility (ECF), ikiwamo kutenga na kutoa fedha katika sekta za huduma za jamii za elimu, afya, barabara vijijini, makundi maalumu, kilimo, maji, umeme vijijini pamoja na kuongeza ajira kwa watumishi kwa sekta za elimu na afya.

Alifafanua kuwa mfumo wa bajeti wa mwaka 2023/24 unaonesha kuwa mapato ya ndani yameongezeka kwa wastani wa asilimia 12, mikopo ya kibiashara ya ndani na nje imepungua kwa asilimia 14.4; matumizi ya kawaida yameongezeka kwa asilimia 10.4, matumizi ya maendeleo yameongezeka kwa wastani wa asilimia moja, bajeti kwa ajili ya



malipo ya madeni yaliyohakikiwa yameongezeka kwa asilimia 129.6.

Kadhalika, bajeti ya miradi ya kielelezo (SGR na JNHPP) imeongezeka kwa asilimia 15.8 na miradi ambayo sio ya kimkakati/kielelezo imepungua kwa asilimia 11.9.

**MISAADA NA MIKOPO**

Waziri alisema misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo inatarajiwa kufikia Sh. trilioni 5.46 sawa na asilimia 12.3 ya bajeti yote huku ikitarajia kukopa Sh. trilioni 5.44 kutoka soko la ndani na Sh. trilioni 3.54 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za serikali zinazoiva na kiasi cha Sh. trilioni 1.89 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

"Serikali inatarajia kukopa Sh.trilioni 2.1 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara, ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu,"alisema.

**DENI LA SERIKALI**

Katika mwaka 2023/24, Mwigulu alisema kati ya Sh. trilioni 29.23 zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zitajumuisha Sh. trilioni 12.77 kwa ajili ya ulipaji wa deni la serikali na gharama nyingine za mfuko mkuu.

**AJIRA MPYA**

Dk. Mwigulu alisema pia kati ya fedha hizo za matumizi ya kawaida Sh. trilioni 10.88 kwa ajili ya mishahara, ikiwamo upandishaji wa madaraja kwa watumishi na ajira mpya.

"Aidha Sh. bilioni 200 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi na wazabuni," alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na maboresho katika sekta ya afya na elimu, uwekezaji mkubwa umefanyika katika ujenzi wa miundombinu, bajeti ya mishahara imeongezeka kutoka Sh. trilioni 9.83 mwaka 2022/23 hadi Sh. trilioni 10.88 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 10.7.

**MIRADI YA MAENDELEO**

Waziri Mwigulu alisema matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 15.15 sawa na asilimia 34.1 ya bajeti yote na kati ya kiasi hicho, Sh. trilioni 11.87 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 78.3 ya bajeti ya maendeleo na Sh. trilioni 3.28 ni fedha za nje.

"Fedha za maendeleo za ndani zinajumuisha Sh. trilioni 1.5 kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha Standard Gauge, Sh. trilioni 1.45 kwa ajili ya kugharamia mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere, Sh. trilioni 1.31 kwa ajili ya Mfuko wa Barabara, Sh. bilioni 899.2 kwa ajili ya mifuko ya reli, maji na REA, Sh. bilioni 528 kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madeni yaliyohakikiwa ya makandarasi," alisema.

Ili kufikia malengo na shabaha za utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24, Mwigulu alisema serikali itaendelea na mikakati na hatua za kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza ikiwa ni pamoja na: kusimamia miongozo ya kubaini vihatarishi katika uendelezaji wa shughuli za kiuchumi ili kuchukua hatua stahiki za kisera na kiutawala kabla, wakati na baada ya kutokea.

Alisema kuimarisha uwezo wa serikali katika kupambana na vitendo vya ukwepaji kodi ikiwamo uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA, udhibiti wa biashara za magendo, utoaji wa elimu kwa mlipakodi pamoja na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato, kutoa unafuu wa upatikanaji wa pembejeo, mbolea, zana za kilimo, viuatilifu, mbegu bora na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji.

"Katika kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbolea nchini, serikali inaendelea kutoa ruzuku ya mbolea na kuvipa kipaumbele viwanda vya ndani vya mbolea katika matumizi ya chokaa ili kupunguza gharama za uzalishaji," alisema.

**TATHMINI BAJETI 2022/23**

Akizungumzia tathmini ya bajeti ya mwaka 2022/23, Dk. Mwigulu alisema katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, serikali ilikusanya Sh. trilioni 22.23 kutoka vyanzo vyote, sawa na asilimia 92.2 ya lengo la Sh. trilioni 24.1.



Anna Henga


**INTERNATIONAL COMMITTEE OF THE RED CROSS**

ICRC

**PUBLIC AUCTION:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** under instructions received from International Committee of the Red Cross, we shall sell two (2) Used Vehicles by public auction on Saturday 25th March, 2023 commencing at 11:00 am. The auction will take place at Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Details of the Vehicles**

| Unit | Make | Model | Year | Duty |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser Hard Top TX | 1HZ Diesel Engine | 2017 | Not Paid |
| 1 | Nissan Qashqai Station Wagon | FDRN Petrol Engine | 2014 | Not Paid |

All Vehicles may be inspected at Golden Resort Sinza, Lion Street, Dar es salaam from March 20th to 24th 2023 from 10:00 am to 4:00 pm.

**AUCTION CONDITIONS:**

1. The winning bidder of the Vehicle must pay immediately 25% of bid amount and the final payment in full within 5 working days by March 31st,2023 at 4:00pm. Payments not made within 5 working days the deposit will be retained by the Seller for breach of Contract.
2. Payments via CRDB and NBC Bank VISA & Master Cards will be accepted.
3. All vehicles are sold on "as is" basis with International Committee of the Red Cross absolving itself from any responsibilities whatsoever.
4. Duty and all taxes are the responsibility of the buyer. All payment of duties, taxes and vehicle registration transfer needs to be completed within a maximum of three (3) weeks' time.
5. Vehicle will only be released to the winning bidder upon proof of duty payments AND vehicle ownership transfer.
6. ICRC has the right to reject the sale partially or completely.
7. All persons entering the premises must obtain a Bid Number at the entrance.
8. All person entering auction yard must wear Mask, Wash hand with running water or sanitizer.

**For further information, contact:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE,**
**(PLOT NO. 5 "E" LION STREET SINZA. DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926 E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

217316602

# MATANGAZO

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
***(AT KINONDONI)***

**CRIMINAL CASE NO**......30..... **OF** 20..23

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**OYSTERBAY HOMES LIMITED**

**To:**

Mohamedraza Akber Tejan
Director / Shareholder
Oysterbay Homes Limited
Plot No. 1872, Oysterbay Area
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the...24... day of ...MARCH.... 20..23..at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this ...06... day of ...MARCH... 20..23...

..........................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name..........................................

Signature..........................................

Qualification/Relationship

Date..........................................

217321102

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
**(AT KINONDONI)**

**CRIMINAL CASE NO**....22..... **OF** 20..23..

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**AMIN HABIB PUNJA**

**To:**

Amin Habib Punja
Plot No. 62, Block M, Magomeni Area,
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the...24... day of ...MARCH.... 20..23.. at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this ...02... day of ...MARCH... 20..23..

..........................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name..........................................

Signature..........................................

Qualification/Relationship

Date..........................................

217321102

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA**
***(AT KIBAHA)***

**CRIMINAL CASE NO.** ...04... **OF** 20...23...

**THE REPUBLIC**
**VERSUS**

**EVANCE DAVID MASUMBIGANA**.....................................**ACCUSED PERSON**

To:
Evance David Masumbigana
Plot No. 21, Block A, Ubena Area
Chalinze District, **Pwani Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the...23rd... day of ...MARCH.... 20..23.. at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 23rd.. day of ...FEB...... 2023..........

..........................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA**

**Served Upon Me/us:**

Name..........................................

Signature..........................................

Qualification/Relationship
Date..........................................

217321102

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
***(AT KINONDONI)***

**CRIMINAL CASE NO**.....30........ **OF** 20..23

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**OYSTERBAY HOMES LIMITED**

**To:**

Ruhaina - Fatema Tejani Lalji
Director / Shareholder
Oysterbay Homes Limited
Plot No. 1872, Oysterbay Area
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the...24th... day of ...MARCH.... 20..23..at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this ...6th... day of ...MARCH... 20..23...

..........................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name..........................................

Signature..........................................

Qualification/Relationship

Date..........................................

217321102

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Matukio ya mauaji, unajisi kamwe yasifumbiwe macho

**MATUKIO** ya mauaji katika maeneo mbalimbali nchini yanayodaiwa yanatokana na tamaa za utajiri, kusafisha nyota na kurithi mali pamoja na ubakaji na unajisi wa watoto wadogo kwa nia kama hiyo, yalikuwa yameshamiri nchini na kuipaka tope Tanzania.

Lakini baada ya kuwapo kwa kampeni kama hizo pamoja na yale ya vikongwe kwa dhana kwamba ni wachawi na yale ya ukataji viungo vya watu wenye ualbino,mambo hayo yalipungua na kuonekana yanatoweka ndani ya jamii. Hali hiyo ilitokana na sheria kuchukua mkondo wake kwa wahusika kufikishwa mahakamani na kuhukumiwa vifungo vikiwamo vya maisha.

Baada ya kuwa hali imetulia, vitendo hivyo vimeanza kurejea kwa kasi. Mkoani Njombe, kwa mfano, Jeshi la Polisi linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kumuua kwa kumnyonga mama yao mzazi, kwa kile kilichodaiwa kutaka kurithi mali.

Licha ya kitendo hicho, mkoani humo pia mtu mwingine anashilikiwa na jeshi hilo kwa madai ya kumnajisi mtoto wa kufikia mwenye umri wa miaka minane kwa madai ya kuondoa mikosi katika biashara na kujipatia utajiri. Mtu huyo ni kwamba hajafanya kitendo hicho mara moja bali kwa muda mrefu, hivyo kumsababishia mtoto athari za kisaikolojia na kiafya kwa kumsababishia maumivu katika mwili wake.

Katika kuthibitisha kukamatwa kwa mtu huyo, Kamanda wa polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema baba huyo amekuwa anambaka mtoto huyo wa kufikia huku suala la ushirikina likihusishwa. Mbaya zaidi, mama wa mtoto huyo, pia amedaiwa kushirikiana na mumewe kwa ajili ya kufanikisha azma yao ya kupata utajiri!

Matukio hayo, hususan la kunajisi watoto wadogo, ni miongoni mwa mengi ambayo yamekuwa yakiripotiwa hivi karibuni katika vyombo vya habari huku yakibainisha kuwa watu wazima wamefikia hatua ya kuwa zaidi ya hayawani kwa kuwaingilia kimwili watoto. Tunasema binadamu wamekuwa zaidi ya hayawani (wanyama au viumbe visivyo na akili ya kutambua jema na baya) kwa sababu hata wanyama hawafanyi hivyo.

Ni vigumu kusikia ng'ombe dume amemwingilia ndama au jogoo kukiparamia kifaranga lakini kwa binadamu linawezakana katika muktadha wa maisha ya sasa kwa sababu umekuwa wimbo wa kawaida vitendo kama hivyo kusikika katika vyombo vya habari. Kwa mantiki hiyo, jamii inajiuliza hivi binadamu amekuwa zaidi ya hayawani?

Sambamba na hilo, suala la mauaji ya wazazi au ndugu kwa ndugu kwa ajili ya kurithi au kugombania mali limeendelea kushika kasi katika maeneo mbalimbali. Jambo hili nalo linazua maswali mengi ikiwamo watu kushindwa kufanya kazi na kutafuta mali zao na badala yake kuvizia mali za wazazi wao na matokeo yake kufikia hatua ya kukatisha uhai wa waliowaleta duniani.

Mambo hayo na mengine ambayo yanafanyika na kukiuka haki za binadamu, ni dhahiri kwamba yanaiweka nchi katika picha mbaya hasa katika uga wa haki za binadamu. Kwa mantiki hiyo, mamlaka zilizopewa dhamana ya kusimamia, kutafsiri na kutekeleza sheria, kwa maana ya polisi, mahakama na wadau wa sheria, zinapaswa kusimama katika nafasi zao na kuhakikisha vitendo kama hivyo vinakomeshwa kabisa.

Si kwamba vyombo hivyo havifanyi kazi, la hasha! Ukweli ni kwamba vinatekeleza ndiyo maana taarifa za watu kufungwa jela maisha ya kufikishwa mahakamani kwa kesi za ubakaji na unajisi zimekuwa zikisikika lakini kinachotakiwa ni kuongeza kasi kwa kuwachukulia hatua wanaodaiwa kushiriki mambo hayo.

Lakini pia jamii inatakiwa kutoa ushirikiano kwa kuwafichua wale wote wanaohusika na vitendo hivyo na hatimaye kuwafikisha katika vyombo vya sheria na kuchukuliwa hatua stahili. Suala la kupinga vitendo vya uovu kama mauaji ya kikatili, ubakaji na ulawiti ni la kila mmoja, hivyo Watanzania wote wanapaswa kushiriki na kuchukua hatua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






### Muungwana Lazima Nilonge

## Hali ya hewa inalazimisha uwezekezaji akiba ya maji

Na Jenifer Gilla

**JUA** ni kali karibu ukanda wote wa pwani kuanzia Pemba hadi Mtwara licha ya wengi kuamini kuwa ungekuwa msimu wa masika. Joto ni kali na upepo unaotikisa karibu nchini kote, huku mkoa wenye Mlima Kilimanjaro, ukigubikwa na jua na joto kali linalofikia nyuzi joto 35, kikiwa ni kiashiria kuwa hali si shwari kwa upande wa mabadiliko ya tabianchi.

Kuna haja ya kufungua macho na kubadilika, zama hizi inaelekea zinahitaji umakini na kuangalia ni wapi kuna tija ili taifa liondokane na uhaba wa chakula na upungufu wa maji unaoathiri, watu, wanyama na mimea.

Jukumu la sasa ni kufanya bidii zote kuwekeza kwenye upatikanaji wa maji ya uhakika kwa kila Mtanzania tena ya kutosha kwa wakazi wa mijini na vijijini ili kila mmoja alime, afuge na apate chakula maana bila uhakika huo, ni vigumu kuzalisha na kuondokana na umaskini, mardhi na njaa.

Hivi karibuni Makamu wa Rais, Dk Phillip Mpango, anasema Tanzania inaweka kipaumbele uwekezaji katika maeneo muhimu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kupata nishati jua na upepo, usimamizi bora wa taka pamoja na teknolojia rafiki kwa mazingira.

Makamu Mpango anayasema hayo wiki iliyopita akishiriki majadiliano ya viongozi wakuu wa mataifa mbalimbali katika ajenda ya mabadiliko ya tabianchi kwenye Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea (LDCs) uliofanyika Doha nchini Qatar.

Pamoja na hayo ni muhimu pia kuwa na mpango kabambe wa kuwa na maji ya uhakika kwa sababu, inavyoelekea kutakuwa na athari nyingi za kukosa chakula kutokana na ukame na jua kali linaloambatana na wadudu waharibifu wa mazao ,mashambani.

Hata kama serikali ilikuwa haijapanga kuingiza juhudi hizo kwenye mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi suala la maji ni muhimu ili kila mmoja azalishe mazao kuanzia mahindi, kunde, mihogo, mboga, matunda hasa matango na matikiti.

**Tanzania inavyofanya juhudi kupanda miti, kulinda vyanzo vya maji na kuhifadhi ardhi juhudi hizo ziende pamoja na kujenga mabwawa, malambo na vihenge vya akiba ya maji.**

Makamu wa Rais anasema Tanzania imeshuhudia matukio makubwa kama vile ukame na mafuriko, hali ya mvua isiyotabirika, kupanda kwa kina cha bahari na baadhi ya visiwa kuzama na kusababisha uhaba wa chakula, migogoro ya kijamii pamoja na kupanda kwa gharama za maisha.

Anaongeza kwamba inakadiriwa kuwa kuna hasara ya kiuchumi hadi kufikia dola milioni 33.7 katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kutokana na mafuriko, yote hayo yanaamsha nia na ari ya kuona namna bora ya kuwekeza kwenye maji na kutoa kipaumbele kwenye sekta hiyo muhimu kwa uchumi, binadamu, kilimo na ufugaji.

Licha ya serikali kukabiliana na hali hiyo kwa kuchimba mabwawa kuhifadhi maji, kuhamasisha nishati safi ya kupikia, upandaji miti kila mkoa, kujenga kingo kando ya bahari kudhibiti mmomonyoko wa udongo, kuandaa mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na mpango kabambe wa mazingira wa mwaka 2022-2032.

Ni wakati wa kuangalia uwezekano wa kuwekeza zaidi katika sekta za maendeleo ya maji pamoja na uhifadhi wa mazingira kwa kutumia teknolojia rafiki kwa mazingira ambayo Watanzania wengi wataimudu.

Ni wazi kuwa uzalishaji hauwezekani kama hakuna maji ya uhakika, hivyo kama kulivyo na vihenge vya nafaka ni wakati pia wa kufikiria kuwekeza kwenye visima, malambo, mabwawa ya maji ambayo yatakuwa akiba siku za ukame mkali unaaonekana sasa.

Tanzania inavyofanya juhudi kupanda miti, kulinda vyanzo vya maji na kuhifadhi ardhi juhudi hizo ziende pamoja na kujenga mabwawa, malambo na vihenge vya akiba ya maji.

# Wahojiwa kuhusu vifo vya watu kula samaki anayedaiwa kuwa na sumu

**Na Julieth Mkireri,** MAFIA

WATU watatu wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Wilaya ya Mafia kwa mahojiano kutokana na vifo vya watu saba vinavyosadikiwa kutokea baada ya kula nyama ya samaki aina ya kasa anayedaiwa kuwa na sumu.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Rufiji, Canute Msacky, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Machi 12, mwaka huu, majira ya saa 1:00 usiku katika kaya nne tofauti wilayani Mafia.

Katika taarifa yake, Kaimu Kamanda huyo alisema watuhumiwa hao nao ni kati ya waliokula samaki huyo na wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mafia wakipatiwa matibabu huku wakiwa chini ya ulinzi.

Aliwataja waliofariki dunia baada ya kula samaki huyo kuwa ni Abdallah Nyikombo (4), Makame Nyikombo (9), Ramadhani Karimu (miezi minane), Minza Hatibu (miezi 10), Salima Mjohi (28), Mohamed Makame (miezi saba) wote wakazi wa kijiji cha Bweni na Ally Selemani (miezi minane) mkazi wa kijiji cha Kanga.

Kamanda Msacky alisema miili ya marehemu imefanyiwa uchunguzi wa kitabibu katika hospitali ya wilaya ya Mafia na kukabidhiwa kwa ndugu kwa taratibu za mazishi na kwamba chanzo cha tukio kinaendelea kuchunguzwa.

Msacky alitoa wito kwa wavuvi kuacha tabia ya kuvua samaki aina ya kasa kwa kuwa ni nyara za serikali na kwamba wanatakiwa kufuata taratibu na sheria za uvuvi wa samaki hao.

Alisisitiza kuwa Jeshi la Polisi linaendelea kuchukua hatua kali kwa wavuvi wasiofuata taratibu na sheria za nchi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania LPG Association, Amos Mwansumbue (kushoto), akizungumza katika semina ya wadau wa gesi ya kupikia LPG, jijini Dar es Salaam jana, iliyojadili mambo mbalimbali kuhusiana na matumizi ya nishati hiyo. Semina hiyo, itaenda sambamba na kongamano kubwa la 'East Africa LPG Expo 2023' pamoja na maonyesho ya bidhaa za gesi ya LPG yanayotarajiwa kufanyika leo na kesho jijini humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapata ufadhili wa BRELA masomo UDSM

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imedhamini wanafunzi watano wanaosomea masomo ya shahada ya uzamili katika miliki bunifu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Hafla ya kukabidhi hundi hiyo ilifanyika jana jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali, wakiwamo wanafunzi waliopata ufadhili huo.

Wanafunzi waliokidhi vigezo na kupata ufadhili huo katika mwaka huu wa masomo ni Grace Mwaikono ambaye ni mtumishi wa Mahakama Kuu na Stanslaus Kigosi ambaye ni mtumishi wa BRELA.

Wengine ni Addo Mwasongwe ambaye ni mtumishi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Erick Mlasani mtumishi wa UDSM na Merciana Ntabaye mtumishi wa UDSM.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa (BRELA), Godfrey Nyaisa, alisema wamechukua hatua hiyo katika kutimiza azma ya kuhamasisha uvumbuzi na ubunifu pamoja na kukuza elimu kuhusu masuala ya miliki bunifu nchini.

Nyaisa alisema ufadhili huo una gharama ya Sh. milioni 16.5 ambazo zinajumuisha ada, gharama za utafiti, shajala, vitabu na posho ya kujikimu kwa wanufaika.

Alisema BRELA imeweka sifa na vigezo ambavyo mdahiliwa anapaswa kuwa navyo ili kupata ufadhili wa masomo tajwa na baadhi ya vigezo hivyo ni pamoja na uraia wa mwombaji, umri, sifa za kitaaluma, hali ya ajira, uwazi kuhusu ufadhili kutoka kwa wafadhili wengine na vilevile kipaumbele hutolewa kuzingatia hali ya ulemavu.

Lengo la ufadhili wa BRELA katika masomo hayo, alisema ni kupanua wigo wa wataalamu katika nyanja ya miliki bunifu kwa kuwa eneo hilo muhimu halina wataalamu wengi nchini.

Alisema lengo lingine ni kuongeza ufahamu kuhusu miliki bunifu kwa maendeleo chanya ya taifa kutokana na umuhimu wa miliki bunifu katika maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii na kuhamasisha wanufaika wa ufadhili kutambua faida zinazopatikana kutokana na elimu kuhusu miliki ubunifu na jinsi ya kuitumia katika kuendeleza, kuhamasisha na kukuza ubunifu.

Kwa mujibu wa Nyaisa, ufadhili huo utasaidia kuweka mkazo mahsusi katika muunganisho wa sheria na sera za miliki ubunifu katika muktadha wa mienendo iliyopo ya kiuchumi na kijamii inayopatikana barani Afrika.

Alisema matarajio ni kuongeza idadi na kuimarisha zaidi wataalamu katika nyanja ya miliki bunifu ili kuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kuratibu mifumo ya miliki bunifu nchini.

Pia alisema matarajio mengine ni kushiriki kikamilifu katika kupitia na kupendekeza maboresho ya sheria zinazohusu masuala ya miliki bunifu ili kuboresha mnyororo mzima wa masuala ya ubunifu na miliki bunifu kwa maendeleo endelevu na kutumia elimu wanayoipata kuwaelimisha wadau na watumiaji wengine wa miliki bunifu nchini ili kujenga utamaduni na uelewa wa masuala hayo.

"Ufadhili wa BRELA katika masomo haya ya MIP utakuwa endelevu kwa wadahiliwa watakaokuwa wanakidhi vigezo vilivyowekwa napenda kutoa rai kwa wanufaika wa masomo ya MIP wanaokabidhiwa hundi zao leo kutumia elimu na maarifa watakayoyapata kutokana na masomo haya kuendeleza na kukuza miliki ubunifu katika maeneo mbalimbali watayotumikia baada ya kuhitimu masomo yao," alisema Nyaisa.

Dk. Sosthenes Materu, Mkuu wa Shule Kuu ya Sheria (UDSM), alisema mwaka 2019 UDSM kupitia Shule Kuu ya Sheria, ilianzisha Progamu ya Shahada ya Uzamili ya Miliki Ubunifu ambayo inatolewa kwa ushirikiano baina ya UDSM na Shirika la Miliki Ubunifu la Kanda ya Afrika (ARIPO), BRELA na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO).

Alisema lengo la kuanzishwa kwa masomo hayo ni kukuza na kuendeleza miliki bunifu nchini na katika kanda na kwamba programu hiyo kwa Afrika Mashariki ni ya kwanza na ya kipekee ambayo inatoa nafasi kwa watahiniwa wa fani zote kujiunga na masomo hayo.

Alisema tangu kuanzishwa kwa programu hiyo, BRELA imekuwa ikitoa ufadhili wa masomo kwa wadahiliwa ambapo mpaka sasa jumla ya wanafunzi tisa ikiwa ni pamoja na wanaokabidhiwa hundi katika hafla hiyo wamenufaika na ufadhili huo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



Minjingu Mines & Fertiliser Ltd.

## TAARIFA KWA UMMA

Uongozi wa Kampuni ya uzalishaji, usambazaji na uuzaji wa mbolea Minjingu Mines and Fertiliser Limited (MMFL) unapenda kutoa ufafanuzi wa tuhuma zilizoelekezwa kwenye Kampuni katika vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii. Tuhuma hizo zilihusu upatikanaji wa mifuko 776 ya mchanga kwenye ghala letu lilloko mjini Njombe. Maelezo yetu ni kama haya yafuatayo:

Kwamba: kampuni ya MMFL ambayo ni kampuni ya uzalishaji wa mbolea aina mbali mbali ni ya Kitanzania iliyojijengea heshima ya uzalishaji na usambazaji wa mbolea ndani na nje ya nchi kwa kipindi cha miaka 22. Tunautaarifu umma kwamba hatujawahi kuhujumu wakulima au wadau wa kilimo kwa kuzalisha na au kufungasha mchanga/udongo katika mifuko yake kama mbadala wa mbolea. Aidha kampuni imeendelea kuwa na ushirikiano wa karibu na Serikali katika kuhakikisha kwamba wakulima wanapata mbolea ya ruzuku kwa wakati na kwa bei nafuu.

Kwamba: Afisa Mauzo wa MMFL kituo cha Njombe -Bwana Gervas John Mtitu alipatikana na upotevu wa mbolea jambo ambalo alilikiri. Baada ya upotevu huo, Bwana Gervas John Mtitu aliendelea kutoonyesha ushirikiano licha ya jitihada mbali mbali za kumtafuta.

Kwamba: baada ya kutoendelea kupata ushirikiano kutoka kwa Bwana Gervas John Mtitu, tarehe 28/1/2023, Kampuni ilitoa taarifa Kituo cha Polisi Njombe mjini kuhusiana na upotevu wa mbolea na kutoonekana kazini ambapo tulipatiwa RB No. NJ/RB/390/2023.

Kwamba: tarehe 20/2/2023, Polisi walifika kwenye ghala na kumweleza Afisa Masoko wa MMFL kwamba walifika kufanya ukaguzi baada ya kupata taarifa kwamba kulikuwa na baadhi ya mifuko ambayo haikuwa na mbolea bali bidhaa nyingine. Katika ukaguzi huo, walibaini kwamba kwenye ile mifuko ya zamani (ambayo iliachwa na Bwana Gervas John Mtitu) , kulikuwa na mifuko yenye mchanga. Afisa Masoko wa Kampuni alichukuliwa na Polisi na ghala kufungwa na kuwa chini ya ulinzi wa Polisi.

Kwamba: tarehe 23/2/2023, maafisa wa TFRA kutoka Kanda ya Mbeya walifika na baada ya hapo, maafisa wa TFRA, Polisi na maafisa kutoka MMFL walifika kwenye ghala na baada ya uchunguzi, walibaini kuwepo na mifuko 776 ya mchanga ikiwa kwenye mifuko ya zamani ya mbolea ya Minjingu. Ili mifuko hiyo ya mchanga kutoonekana kiurahisi, mifuko ya mbolea halisi (ile ya zamani) ilizungushwa pande zote ili ionekane kwamba yote ilikuwa mbolea.

Kwamba: TFRA waliiandikia MMFL barua tarehe 24/2/2023 ambapo maudhui ya barua ilikuwa ni kukutwa na bidhaa ambayo siyo mbolea na Kampuni ilipigwa faini ya shilingi milioni 30. Kampuni ililipa faini hiyo tarehe 25/2/2023.

Kwamba: MMFL imesikitishwa suala hilo (ambalo Mamlaka inayohusika Kisheria ilishalitolea maamuzi) kuletwa tena tarehe 5 Machi 2023 kwenye jamii na kuleta sintofahamu kwa jamii.

Kwamba: katika jitihada za kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kulingana na uhitaji wa virutubisho wa zao, MMFL imekuwa ikishirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) na kutokana na jitihada hizo, Kampuni imeweza kuzalisha mbolea maalum kwa ajili ya mazao ya chai, kahawa, tumbaku, pamba na mazao ya chakula.Tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na Taasisi za Utafiti ili mazao mengi zaidi yaweze kuwa na mbolea zinazokidhi mahitaji ili kuongeza tija.

Kwamba: kutokana na ubora wa mbolea zetu, Kampuni imekuwa ikiuza mbolea zake Kenya, Burundi, Rwanda na Uganda na hakujawahi kuwa na malalamiko yanayohusiana na ubora wa mbolea na mahitaji kwenye nchi hizo yamekuwa yakiongezeka.

**Hivyo:**

- Tunawahakikishia wakulima wote wa Tanzania kwamba Kampuni ya MMFL itaendelea kuwapatia wakulima mbolea zenye ubora.
- Tuko tayari kushirikiana na vyombo vya dola katika kuhakikisha kwamba mtuhumiwa anapatikana na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria.
- Kampuni inaamini kwamba mhusika atakapopatikana, atasaidia kutoa taarifa ambazo zitasaidia kujua kama haya yaliyojitokeza ni jitihada za yeye peke yake au kuna hujuma ili kuidhoofisha kampuni ya MMFL.

**Tunamhakikishia Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – DKt Suluhu Samia Hassan na Serikali yote kwamba Kampuni ya MMFL itaendelea kuwahudumia wakulima wa Tanzania na wa nchi ambazo wanatumia bidhaa zetu kwa kuwapatia mbolea zilizo na ubora.**

**Imetolewa na :-**
**Kurugenzi ya Mawasiliano**
**Minjingu Mines & Fertiliser LTD**

# BoT yaongeza mwezi mmoja usimamizi Yetu Microfinance

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imeongeza muda wa usimamizi wa Yetu Microfinance Bank kwa mwezi mmoja mwingine.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwenye vyombo vya habari, iliamua kuchukua usimamizi wa benki hiyo tangu Desemba mwaka jana baada ya kubaini ilikuwa na upungufu wa ukwasi na mtaji kinyume na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake.

"Itakumbukwa kwamba, kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha sheria namba 56(1) (g) (iii) cha sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania, iliamua kuchukua usimamizi wa Yetu Microfinance Bank kuanzia Desemba 12, mwaka jana baada ya kubaini kuwa ilikuwa na upungufu mkubwa wa ukwasi na mtaji kinyume na matakwa ya sheria ya mabenki na taasisi za fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake," ilieleza taarifa ya BoT.

"Baada ya kuchukua usimamizi wa benki hii, BoT ilisitisha shughuli za utoaji wa huduma za kibenki za benki hiyo kwa muda wa siku 90 ili kuipa nafasi kutathmini hatua za kuchukua kupata ufumbuzi wa suala hilo.

"BoT inapenda kuuarifu umma kuwa mchakato wa kutathmini hatua za kuchukua, ili kupata ufumbuzi wa matatizo ya Yetu Microfinanc Bank haujakamilika, hivyo muda wa usimamizi umeongezwa kwa kipindi cha siku 30 Machi 12, mwaka huu."

"BoT inauhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenye amana katika mabenki kwa lengo la kuleta ustahimilivu sekta ya fedha."

# Wanawake wafundwa kutokuchagua kazi

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE nchini wametakiwa kuacha kuchagua kazi badala yake wachangamkie fursa zinazojitokeza ambazo wana uwezo wa kuzifanya kwa ufanisi, zikiwamo zile zinazoitwa za wanaume hususani udereva wa magari makubwa hasa malori.

Wito huo umetolewa kutokana na kuthibitika kwamba wanawake wana uwezo sawa na wanaume kufanya kazi yoyote na miongoni mwao wanafanya vizuri zaidi ya wanaume.

Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni za Bravo Logistics na Agricom Africa, Angelina Ngalula, alisema hayo jana katika hafla fupi ya kuwapongeza madereva wanawake wa kampuni hizo kwa kazi nzuri na uwezo walioonyesha kuliko madereva wanaume.

Ngalula ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), alisema kwenye kazi na biashara hakuna kazi za wanawake wala za wanaume bali kanuni ni moja tu ya kufanya mambo kwa juhudi na maarifa na hatimaye kupata matokeo bora ikiwamo kuzalisha faida.

Kuhusu uwezeshaji wa upendeleo kwa wanawake, Ngalula alipingana na kauli kwamba "wanawake wakiwezeshwa wanaweza" na kusisitiza kwamba wanawake wana uwezo na wanaweza kwa sababu wana uwezo sawa na wanaume na wengine hata kuwazidi.

"Ili wanawake waonyeshe kuwa wana uwezo, kitu wanachohitaji si nafasi za upendeleo au kubebwa, bali wajengewe uwezo kwa kuwezeshwa kimtaji, ikiwamo mikopo, kuwekewa mazingira bora ya biashara na kufunguliwa fursa za masoko, kitu ambacho hata wanaume wanahitaji," alisema.

Ngalula alijitolea mfano wake kwamba japo ni mwanamke, anamiliki kampuni ya usafishaji ya malori ya masafa marefu ya Bravo Logistics na kampuni ya zana za kilimo ya Agricom Africa, inayojihusisha na uuzaji wa matrekta.

Alisema kampuni zake zinafanya kazi zinazodaiwa kuwa ni za wanaume lakini ameingia huko bila kuwezeshwa kwa mikopo ya upendeleo, hivyo kusisitiza wanawake wana uwezo sawa na wanaume na wengine wana uwezo kuliko wanaume.

Ngalula pia alisema Rais Samia Suluhu Hassan anaonyesha uwezo kwenye baadhi ya mambo kwa kuyaweza mambo mengi ambayo awali yalionekana yanaweza kufanywa kwa ufanisi na wanaume hasa uongozi wa nchi. "Rais Samia ameonyesha kwa vitendo kuwa wanawake wanaweza na hawa wanawake waliowekwa katika nafasi mbalimbali za uongozi serikalini na kwenye taasisi wameonyesha kuwa wana uwezo mkubwa,' alisisitiza.

Wakitoa ushuhuda wa kazi ya udereva wa malori ya masafa marefu kwa madereva wanawake, madereva Asha Mkumba, Mosi Msengwa na Mwajuma Mhando walisema kazi hiyo ni sawa na nyingine yoyote na kwamba madereva wanawake wanaifanya vizuri sawa na wanawake na hata kuwazidi.

Walisema changamoto pekee ya kazi ya udereva wa malori kwa wanawake mfumo dume. Walisema licha ya kufanya kazi, bado wanakabiliwa na majukumu ya kifamilia kama mama wa familia kwa mwenza wake hali ambayo huwafanya kupata muda mfupi wa kukaa nyumbani kuangalia familia.



**HABARI KANDA KASKAZINI**

## MABOA wampa 5 Chongolo kurudisha magari stendi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi mkoani Manyara (MABOA) kimempongeza Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, kwa kuiagiza serikali kurudisha magari madogo kutoa huduma katika stendi ya zamani.

Kaimu Mwenyekiti wa MABOA, Salimu Ngobezi, alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa wanamshukru Chongolo kwa kusikia kilio chao cha muda mrefu.

Alisema kuondolewa kwao katika stendi hiyo miaka sita iliyopita ilikuwa ni kilio cha wamiliki wa mabasi, wafanyabiashara wenye vibanda, wananchi na mama lishe.

Aidha, alisema walinyanyaswa kwa ajili ya migongano ya viongozi lakini kwa sasa ameomba wawaache wafanye kazi kwenye eneo zuri ambalo liko katikati ya mji kwa kuwa linafikika kiurahisi.

Mwenyekiti wa madereva wa njia ya Babati na Gallapo, Shisha Mushi, alisema ameshangaa kuona imeanzishwa stendi kuu lakini wanakosa stendi ndogo ya magari madogo.

"Tunaomba suala hili lisije likaingiliwa tena agizo limeishatoka utekelezaji uendelee,"alisema Mushi.

Mmiliki wa magari, Festo Sandu, alisema watu wengi waliathirika na walishindwa kufanya biashara ya usafirishaji na waliuza magari kwa kuwa mtu aliyenunua gari kwa Sh. milioni 20 alifilisika na kuliuza kwa Shilingi milioni nne.

"Viongozi tunaomba waache malumbano ambayo hayana tija watuache tufanye kazi sisi tuko tayari kulipa ushuru wowote wanaotaka,"alisema Sandu.

Naye Chiku Shaban, alisema wanamshukuru Katibu Mkuu wa CCM kwa kuruhusu magari madogo yatoe huduma za usafirishaji kuanzia stendi ya zamani.

Alisema kuhama kwa stendi hiyo kumesababisha watu wengi kushindwa kulipa mikopo.

Nyange Polepole, alisema stendi ilipohamishwa waliathirika kiuchumi na wateja wao walikimbia, hivyo biashara ziliyumba lakini kutokana na agizo la Chongolo watakwenda kufufua biashara.

Mfanyabiashara wa mafuta, Bakari Yahya, alisema wamefarijika na uamuzi uliotolewa na Chongolo kwa kuwa walikuwa hawapati wateja ila kwa sasa watapatikana.

Machi 10, mwaka huu Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, akihitimisha ziara yake mkoani Manyara, katika Halmashauri ya Mji wa Babati, aliwaagiza viongozi wa halmashauri hiyo na mkoa kuruhusu magari madogo yarudi stendi ya zamani, ili kutoa huduma za usafirishaji na ushuru utozwe na halmashauri.

# ADC yatoa sifa lukuki miaka miwili ya Samia madarakani

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

CHAMA cha ADC kimesema miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kimeleta taswira mpya katika masuala mbalimbali, ikiwamo eneo la siasa inayofuata misingi ya demokrasia.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Doyo Hassan Doyo, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe, kueleza kuwa katika uongozi wa Rais Samia Tanzania imeshuhudiwa ikipiga hatua kubwa kimaendeleo ikiwamo kufunguka kidiplomasia kimataifa.

"Kwenye eneo la demokrasia nchini hapo amefanya mambo makubwa, sote tunashuhudia hivi sasa siasa kwa vyama vyetu vya upinzani zikiamka upya tofauti na ilivyokuwa hapo nyuma, kila chama sasa kimepewa uhuru wa kufanya siasa, hili ni jambo kubwa ambalo chama chetu kinampongeza," alisema Doyo.

Alisema awali Tanzania ilikuwa kama ipo gizani kutokana na kujitenga kwake na masuala mbalimbali likiwamo kuweka mazuio ya kila aina, ila tangu aingie madarakani Rais Samia amebadilisha upepo huo na kuirejesha katika mstari.

Doyo alisema mambo mengi aliyoyafanya Rais Samia katika kipindi hicho yanapaswa kupongezwa na Watanzania wote kwa kuwa yameiletea Tanzania matunda na kumfanya kila mtu kijivunia uwapo wake madarakani.

"Rais Samia Suluhu Hassan kwa kiasi kikubwa amewaonyesha Watanzania ukomavu wa kisiasa, ametoa vikwazo mbalimbali ambayo sisi wanasiasa yalitufanya tushindwe kufanya siasa zetu, hili ni eneo muhimu ambalo sote tunajua kuwa kama hujapewa nafasi ya kulifanya ni sawa na kutokuwapo chama," alisisitiza Doyo.

Kuhusu ushirikiano wa kimataifa, Doyo alisema ndani ya miaka miwili imeshuhudiwa Tanzania ikitembelewa na viongozi wa kimataifa.

Alisema ujenzi wa miundombinu ikiwamo ya reli ya kisasa (SGR), barabara, madaraja, shule, hospitali, kuongeza mishahara ya wafanyakazi ni mambo yanayowafanya Watanzania kuzidi kujenga imani naye.




Diwani wa kata ya Bomambuzi, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Juma Raibu akizungumza na wananchi wa kata hiyo, eneo la Soko la Pasua juzi, kuhusu kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia na kupigania haki za watoto wakati akisikiliza kero mbalimbali za wananchi hao. **PICHA: JAMES LANKA**

# Watalii kutoka Ufaransa wafanya ziara mgodi wa tanzanite

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WATALII 17 kutoka Ufaransa wamefanya ziara katika mgodi wa kuzalisha madini ya tanzanite uliopo eneo la kitalu C unaomilikiwa na Kampuni ya Franone Mining, iliyoko Mji wa Mirerani, wilayani Simanjiro mkoani Manyara.


Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya ziara hiyo, watalii hao walisema wamefurahi kuona sehemu pekee inayochimbwa madini ya tanzanite.

Akizungumza baada ya kuwapokea watalii hao, Meneja Mkuu wa Kampuni ya Franone Mining, Vitus Ndakize, alisema wamesikia faraja kutembelewa na wageni hao.

"Kitendo cha watalii hawa kufika kwenye mgodi wetu, kimekuwa ni faraja kwa kuwa tumeweza kujifunza mengi kutoka kwao na tumeweza kuweka historia kwa kutembelewa na kundi hili ambalo wameweza kujionea namna ya utendaji kazi wetu," alisema. Aidha, aliishukuru Wizara ya Madini kwa kuwakaribisha watalii hao akisema ujio wao unaendelea kuitangaza Tanzania, kuwa ndiyo sehemu pekee madini ya tanzanite yanapatikana.

Aidha, alisema kwa sasa mgodi huo umeanza kazi rasmi na wanategemea kuwa na uzalishaji mkubwa kutokana na wataalamu wa miamba kutoka maeneo ambayo madini yanapatikana licha ya kwamba mgodi huo haukufanya kazi kwa muda wa miaka mitano.

Mmoja wa watalii hao, Camille Constant, alisema amepata uzoefu wa uchimbaji wa madini ya tanzanite, hivyo atakuwa balozi mzuri kwa wenzake pamoja na watalii wengine.





# Wakufunzi wanaotoa mbinu za kufanya uhalifu kushughulikiwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imesema itachukulia hatua za kisheria wanafunzi waliohitimu mafunzo ya utunzaji na uhifadhi wa rasilimali za misitu watakaobainika kujihusisha na vitendo vya ujangili pamoja na kutoa mbinu za uhalifu.

Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Dinna Mathamani, alitoa kauli hiyo wakati wa kufunga mafunzo ya muda mfupi katika Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasians.

Alisema kuwa hali hiyo imekuwa ikizidisha vitendo vya ujangili katika hifadhi mbalimbali nchini. Alisema kumekuwa na baadhi ya wahitimu wa mafunzo wasiowaaminifu kutumia vibaya ujuzi wanaoupata na kujihusisha na vitendo vya ujangili, hivyo serikali haitasita kuwachukulia hatua za kisheria.

Kadhalika aliwataka wahitimu hao kuyatumia mafunzo waliyopewa kulinda rasilimali za misitu na maji.

"Tukitanguliza uzalendo mambo mengine yanayotokea katika hifadhi hayatojitokeza tena na msipokuwa makini serikali haitowavumilia maana uwezo wa kuwabaini upo," alisema.

Mkuu wa Chuo cha Taaluma ya Wanayamapori, Jeremiah Msigwa, alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuwawezesha askari hao pamoja na wananchi kukabiliana na matukio ya ujangili yanayojitokeza katika maeneo yao.

Alisema ujasili na uzalendo vinahitajika ili kuhakikisha hifadhi zinakuwa salama wakati wote ikiwa ni pamoja na kutunza hifadhi za taifa, ili ziendelee kuwa kuvutio kwa watalii na kuendelea kuliingizia taifa fedha za kigeni.

Mshauri wa Misitu na Maliasili kutoka Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (FZS), Hassan Chikira, alisema wataendelea kushirikiana na serikali katika kuwajengea uwezo wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi ili kuifanya sekta ya uhifadhi kuwa endelevu.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni (kushoto), alipotembelea banda la Vodacom, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani 2023 kwenye viwanja vya Furahisha jijini Mwanza jana. Wengine ni Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima (katikati) na Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillus Wambura. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC akemea vitendo vya ukatili dhidi ya watoto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amelaani vitendo vya ukatili dhidi ya watoto mkoani hapo.

Alitoa tamko hilo juzi wakati akizungumza na wazee wa Manispaa ya Shinyanga, ikiwa ni siku yake ya kwanza kufanya kazi mkoani humo tangu ateuliwa na Rais Samia.

Alisema analaani vitendo vya ukatili ambavyo vimekuwa vikiendelea mkoani Shinyanga na kuwaomba wazee wasimamie mmomonyoko wa maadili ya vijana kwa sababu kwa sasa wamekiuka mila na desturi.

"Ninyi wazee mlitusimamia sisi katika maadili mema, lakini siku hizi maadili ya vijana wetu yamekwisha kabisa, naomba mtusaidie na kuisaidia serikali kumaliza matukio haya ya ukatili dhidi ya watoto wadogo wakiwamo na wazazi kulawiti watoto wao,"alisema Mndeme.

Aliongeza: "Hapa Shinyanga siku siyo nyingi alikamatwa mzazi akilawiti watoto wake wawili na alikuwa akiwafanya kila siku mmoja ana miaka nane na mwingine 11, ila nashukuru kwa sasa anashikiliwa na polisi na tutahakikisha anachukuliwa hatua kali za kisheria na hili litakuwa funzo kwa wengine,"aliongeza.

Aidha, aliwaahidi wazee mkoani humo kuwa ataendelea kuwaboreshea huduma bora za matibabu, kwa kutengewa madirisha yao kwenye huduma zote za afya, upatikanaji wa dawa.

Katibu wa Baraza la Wazee mkoani Shinyanga, Anderson Lyimo, alimpongeza Mndeme kwa kukutana na wazee siku yake ya kwanza na kumwahidi kumpatia ushirikiano na kuchochea maendeleo.

Pia alitaja baadhi ya matatizo ambayo bado huwakabili wazee na kuiomba serikali iyashughulikie, likiwamo suala la ukosefu wa dawa kwenye baadhi ya vituo vya afya, wazee kutoshirikishwa kwenye vikao vya maamuzi hasa ngazi ya halmashauri, kutotengewa bajeti pamoja na kutelekezwa.

# TRA yatangaza zawadi kwa watakaofichua wakwepa kodi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

OFISA Elimu na Huduma kwa Mlipakodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kahama, Aniceth Ndailagije, amewataka wafanyabiashara wilayani humo kuwafichua wenzao wanaokwepa kulipa kodi na kusababisha malimbikizo.

Amesema mfanyabiashara atakayefanikisha hilo atapewa zawadi ya fedha kiasi cha asilimia tatu kulingana na kodi itayokuwa imeokolewa. Alibainisha hayo jana wakati akitoa elimu ya mlipakodi kwa wafanyabiashara hao, kuwakumbusha kutokulipa kodi kwa wakati kunasababisha kupigwa faini na riba kuongezeka.

Kodi hizo ni pamoja na Ongezeko la Thamani (VAT), kodi ya zuio pamoja na kodi ya wafanyakazi au ajira (PAYE) ambazo zimekuwa hazilipwi kwa wakati na kusababisha kuwapo kwa malimbizo makubwa ya madeni na riba kuongezeka.

Alisema kazi ya TRA siyo kuwatoza riba na kuwapatia adhabu wafanyabiashara, bali wanawakumbusha kuepukana na adhabu kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kufanya biashara na kulipa kodi kwa wakati.

"Atakayemfichua mfanyabiashara anayekwepa kodi kuna kiwango cha fedha atalipwa na TRA cha asilimia tatu ya kiwango kitakacholipwa na mdaiwa na hakiwezi kuzidi Sh.milioni 20. Tufanye biashara kwa kushirikiana kwa sisi sote tunategemeana katika kazi,"alisema Ndailagije.

Kaimu Meneja wa TRA Kahama, Honest Mushi, alisema mkoa wa kikodi Kahama umekuwa kinara katika kutozilipa kodi hizo kwa wakati kulinganisha na mikoa mingine.

Aidha kwa kutoziwasilisha kunasababisha kuwa na malimbikizo ya kodi, wakati mwingine wanalazimika kuzitumia katika mambo yao binafsi ya kibiashara na kuwaomba kuacha tabia hiyo.

Mushi alisema wafanyabiashara wakubwa hutozwa kodi katika faida wanazozipata, huku wale wakati wakitozwa kodi katika mauzo yao, hivyo kila mmoja anawajibu wa kutunza kumbukumbu za mauzo.

Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara (TCCA) wilayani hapo, Charles Machali, alishukuru TRA kwa kuendelea kuwapatia elimu ya kodi na kuahidi kuyasimamia na kuyafanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuwafichua wote wasilipa kodi hizo kwa wakati.

Mwakilishi wa Shirika la SHDEPHA+, Janeth Syprian, alisema wafanyabiashara wengi hawaoni umuhimu wa kulipa kodi kwa sababu wanakosa elimu ya masuala hayo.

Hivyo aliiomba TRA kuendelea kutoa elimu kuhusu ulipaji wa kodi ili wafahamu umuhimu na madhara yake.



Ukurasa 12

Chongolo anapowamwagia upupu wapenda kupigiwa makofi na porojo



Ukurasa 13

**VOLKANO YALIPUKA TLP 'Mzimu' wa Mrema unapokwamisha kuchagua wa kumrithi, mambo yakiahirishwa kiaina**



Ukurasa 14

**BOLA AHMED TINUBU Ndiye rais ajaye Nigeria, kuapa Mei 29, ni bepari ila chanzo utajiri hakijulikani**


# siasa

JUMATANO MACHI 15, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


NDICHO RAIS SAMIA ANACHOAKISI

# Utofauti, umahiri kati ya kiongozi mwanaume na mwanamke kwenye kushughulikia mambo

**Na Restuta James**

JUMATANO iliyopita, dunia imesikia kinamama wakitoa ya rohoni, ni kwenye maadhimisho siku ya Kimataifa ya Wanawake yenye kauli mbiu 'Ubunifu na Teknolojia, Chachu ya Usawa wa Kijinsia.'

Wanawake wa kada mbalimbali wanapaza sauti zao wakieleza namna ambavyo teknolojia ikitumika kikamilifu inaweza kumkwamua mwanamke na jamii kwenye umaskini.

Pamoja na mengi yanayozungumzwa kuhusu teknolojia, wanawake Tanzania wanamwangalia mwanamama, mkuu wa nchi, Rais Samia Suluhu Hassan, kwa namna ya kipekee.

Anaanza, mwanaharakati wa Haki za Binadamu Dk. Helen Kijo-Bisimba, anayemtaja Rais Samia kama mwanamke wa shoka na wa kuigwa, akisema utendaji wake umedhihirisha utofauti wa namna ya kushughulikia mambo kati ya kiongozi mwanaume na mwanamke.

Anasema wakati wa uchaguzi mkuu wa vyama vingi mwaka 1995, mfumo huo ulichukuliwa kama ni uadui, dhana ambayo anasema awamu ya Rais Samia inaifuta.

"Hatua ya mkuu wa nchi na Mwenyekiti wa CCM inayoongoza dola kujumuika kwenye jukwaa la wanawake wa chama cha upinzani CHADEMA, imeongeza maana kubwa zaidi kwa ustawi wa nchi na utengamano kati ya siasa na maridhiano nchini.

Itakumbukwa kwamba, Jumatano iliyopita, Rais Samia alijumuika na kuwa mgeni rasmi kwenye mkutano wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA), mkoani Kilimanjaro, ambako alialikwa kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani.

Anasema pamoja na kwamba mfumo wa vyama vingi vya siasa ni suala la kikatiba, katika hali ya utendaji mambo ni tofauti kwani umekuwa kama uadui.

"Nimemsikia anasema anataka kujenga nchi iliyo pamoja, na ndivyo inavyotakiwa. Taifa gani unaishi unaogopa kuingia kwenye vyama hasa upinzani?"Anahoji.




Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea Tuzo ya Maridhiano kutoka kwa Mwenyekiti wa CHADEMA Freeman Mbowe, akiikabidhi kwa niaba ya BAWACHA. **PICHA: CHADEMA**

### TOFAUTI KIUONGOZI

Dokta Hellen anamsifu Rais kuwa ni kiongozi wa raia wote hivyo anawajibika kuwakumbatia wote bila kujali itikadi za vyama, dini wala makabila.

"Anachofanya Rais nimemfurahia na nikasema ametuonyesha tofauti ya uongozi kati ya mwanamke na mwanaume na hii inaweza kumjengea msingi madhubuti, umahiri na heshima kubwa sana," anasema mwanasheria huyo aliyeongoza Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

Anagusia kufufua mchakato wa katiba akieleza kuwa anatamani Rais Samia aongoze ajenda hiyo na kuihitimisha kwa manufaa ya nchi akisema:

"Ningetamani aliongoze hilo ili aweke alama ya Rais mwanamke kwamba ameweza kufanya kitu kama hiki. Atuletee jambo la kitofauti, mbadala na vitu ambavyo vimewahi kutokea."

### MIAKA 2 UONGOZINI

Anazungumzia miaka miwili ya Rais Samia madarakani akisema anaingia kuongoza nchi wakati muafaka, tena katika kipindi kigumu na kwamba kile ambacho wananchi walikihitaji amekifanya.

"Kwa ile hali ambayo tulikuwa tumefikia, nadhani alikuwa ni mtu muafaka mwenye kuleta suluhu na kusawazisha ili hali iwe bora" anasema.

Anaongeza kuwa Rais Samia amefanikiwa kuachia baadhi ya watu ambao walikuwa wamefungwa na kurudisha akaunti za fedha zilizokuwa zimefungwa jambo ambalo anaeleza kuwa ni zuri na ni haki ya watu.

Hata hivyo, anasema wananchi wana mambo ambayo wangetamani yafanyike haraka na kwamba ni kwa kuwa wameyadai kwa muda mrefu.

"Suala kama la katiba na sheria mbaya ziondolewe. Tunatamani kama anaweza afanye sasa maana akija mwingine tunaweza tukarudi kule kule. Kwa hii miaka miwili tumekuwa na uhuru fulani mzuri sana," anasema.

Kuhusu maendeleo, Dk. Hellen anasema miradi mikubwa inaendelea kutekelezwa jambo ambalo linadhihirisha kwamba mwanamke anaweza kufanyakazi kwa ukamilifu na utimilifu.

Anaeleza kuwa pamoja na kwamba baadhi ya watu wanalalamikia mikopo inayochukuliwa na serikali, utekelezaji wa miradi mikubwa unaonyesha fedha hizo zinakopelekwa na si mikopo kwa hasara.

"Tukiweza kupata umeme nchi nzima kitakuwa ni kitu kizuri kama ambavyo tunaona mtandao mkubwa wa barabara za lami. Tulikuwa tunaambiwa tutatoka Mtwara kwa barabara hadi Bukoba tukawa tunashangaa lakini vitu kama hivyo vinawezekana," anasema.

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawenza, anampongeza Rais Samia kwa kuongea na wanawake kupitia jukwaa la BAWACHA, akisema ni chachu ya kuleta mabadiliko ya uongozi ndani ya jamii.

Anasema kitendo hicho kinajenga mahusiano bora miongoni mwa wananchi na kwamba kitaamsha nguvu ya mashauriano na kuwaleta Watanzania pamoja na kwamba amekwenda kuimarisha ustawi wa vyama vya siasa nchini na amekuja kuimarisha mahusiano yanayojengeka katika misingi ya uongozi bora katika nyanja zote.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Wakiislam Tanzania, Shamim Khan, anapongeza hatua hiyo ya Rais Samia akieleza kwamba amefanya kitendo cha kidemokrasia ambacho ni cha kudumu.

"Ndiyo demokrasia; yeye kachaguliwa na wanawake wote

INAENDELEA UK.12

# Chongolo anapowamwagia upupu wapenda kupigiwa makofi na porojo

**Na Augusta Njoji, SINGIDA**

CHAMA Cha Mapinduzi, kimetangaza kuangalia mienendo ya makada na viongozi wake, safari hii kikiwaonya kuwa hakitakubali wanaopenda kupigiwa makofi wakati wananchi wanateswa na kero mbalimbali.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo ameyasema hayo katika ziara ya siku sita mkoani Singida, akiambatana na sekretarieti ya chama hicho kuzungumza na wananchi kusikiliza kero na kuzitatua.

Anaongeza kuwa sifa ya kiongozi ni kuzungumzia matatizo na kuyatafutia ufumbuzi na kwamba CCM imepewa dhamana ya kuongoza nchi na viongozi hawaji kupiga porojo ila kusikiliza watu, kuchukua changamoto na kuzitatua na huko ndiko kuhangaikia mambo ya wananchi.

Katika ziara hiyo inayolenga kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025, anatembelea mashina ya CCM ili kuangalia uhai wa chama, ukaguzi wa miradi ya maji, vituo vya afya, hospitali na ujenzi wa miundombinu mkoani Singida.

**MBOLEA YA RUZUKU**

Akiwa Singida, Chongolo anapokea malalamiko ya mbolea ya ruzuku na kueleza kuwa CCM imetuma wachunguzi maeneo yaliyolalamikiwa kwenye ugawaji wa pembejeo ikiwamo mbolea.

Anasema Rais Samia Suluhu Hassan aliamua kuwapunguzia mzigo wa gharama za pembejeo ambazo ni mbegu, mbolea na dawa za viuatilifu kwa kutoa ruzuku ya zaidi ya Shilingi bilioni 150.

Aidha, kwenye ziara hiyo anakishukia Kituo cha Uwekezaji (TIC) kwa kuishia kuwasajili wawekezaji kwenye makabrasha badala ya kuwatembelea kujua kero zao na kuzitatua ili uwekezaji uwe na tija kwa taifa.

Akikagua mradi wa kilimo cha alizeti unaotekelezwa na Kampuni ya Alfardaws, anasema kituo hicho kina jukumu la kutoa kibali kwa wawekezaji na kuhakikisha mahitaji muhimu yanamfikia kwenye eneo lake lakini hawafanyi hivyo.

"Bado tumeshindwa kutoka kuwa watu wenye kutimiza wajibu kuwa watu wenye kutafuta matokeo lazima kama nchi hili tulifanye kwa dhati ya mioyo yetu, hatuwezi kuwa na namba ya wawekezaji tuliowasajili hatujui huko wanafanya nini, wanawezeshwaje kufikia uwekezaji uliokusudiwa,"anasema.



Katibu Mkuu wa CCM, akiwa jukwaani mkoani Singida hivi karibuni. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

> "Nakwenda kukaa na Waziri wa Afya aniambie mpango wa MSD kupeleka dawa na vifaa tiba kwenye hospitali na vituo vya afya vilivyojengwa n, majengo yakikamilika yanapaswa kutoa

Katibu huyo anasema mwekezaji Alfardaws kwa zaidi ya miezi minne ana tatizo la kutounganishiwa umeme ambao upo kilometa tatu na kutaka viongozi kutimiza wajibu.

Akiwa mgodi wa dhahabu Shanta, anasema kumekuwa na tatizo la umeme kwa wawekezaji na kuitaka Tanesco kuweka msukumo wa kujenga vituo vya kupoozea umeme kwenye maeneo yenye uwekezaji mkubwa ikiwamo ukanda wa Singida.

**UKATILI KIJINSIA**

Chongolo anaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuweka mfumo wa kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa jamii baada ya wananchi wa maeneo ya Singida kulalamikia kukithiri kwa vitendo hivyo.

"Hatuwezi kuwa na nchi ambayo inaacha matendo ya ukiukwaji wa haki za binadamu na sisi tukasema tupo na amani ni lazima matendo haya yashughulikiwe hata kama ni machache."

Anatoa maelekezo kwa Wizara ya Afya ibainishe mpango wa Bohari ya Dawa (MSD) wa kupeleka dawa na vifaa tiba kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati zilizojengwa ili kuhudumia wananchi.

"Nakwenda kukaa na Waziri wa Afya aniambie mpango wa MSD kupeleka dawa na vifaa tiba kwenye hospitali na vituo vya afya vilivyojengwa n, majengo yakikamilika yanapaswa kutoa huduma,"anakumbusha.

Katika hatua nyingine,anamtaka Mwenyekiti wa Halmashauri ya Singida, Elia Diga kutoa majibu kwa wananchi kuhusu kulazimishaa kulipa fedha za matibabu kabla ya kupata huduma.

Akiwa katika Kijiji cha Mntiko, anapokea malalamiko hayo ambayo mkazi wa kijiji cha Mtinko, Jamal Kyoka, anasema wanapokwenda hospitali mtu anatakiwa kutibiwa ndipo alipe fedha lakini kwasasa mgonjwa asiye na fedha anakuwa hatarini.

Anasema anaweza kufia kwenye benchi kwa kuwa hatapewa huduma bila kutoa fedha kwanza, ndipo

Katibu Mkuu Chongolo anaposema wananchi wapate huduma kisha walipe, akimtaka mwenyekiti huyo kuondoa malalamiko hayo kwa wananchi.

**KWA SERIKALI**

Akihitimisha ziara anatoa maelekezo manne kwa serikali baada ya kubaini kero mbalimbali zinazowakabili wananchi kwenye sekta ya afya, elimu na kilimo.

Anaelekeza hospitali zinazojengwa wilayani na zilizokamilika zianze kutoa huduma kwa wananchi ili kuzuia vifo vya mama na watoto.

Anasema CCM inaelekeza serikali na kuweka msukumo wa kuhakikisha wahudumu wa afya wanaletwa kwa idadi ya kutosha ili huduma zitolewe kwenye hospitali hizo ili kuleta matokeo halisi yaliyokusudiwa ya kusogeza huduma kwa wananchi.

Pia anasema kuna baadhi ya maeneo fedha kutoka serikali zimechelewa kumalizia majengo ya zahanati yaliyojengwa na fedha za wananchi ikiwamo Kijiji cha Ngimu, Kinambeu na kutaka serikali ipeleke fedha haraka ili kukamilisha. ujenzi.

Kuhusu sekta ya elimu, anaeleza kujenga shule za kidato ya tano na sita ndani ya miezi mitatu ili kupanua wigo wa kupokea wanafunzi kutoka asilimia 25 hadi 70.

Akizungumzia kuhusu kilimo, anasema mkoa huo unalima kwa kiwango kikubwa alizeti ili kupunguza utegemezi wa mafuta ya kula kutoka nje hivyo wajibu wa serikali ni kulinda bei ya mafuta na wakulima wa alizeti kwa kuzuia uingizaji wa mafuta bila kufuata taratibu.

Anawahakikishia kuisukuma serikali na kuwajibika kupeleka pembejeo za mbolea ya ruzuku kwenye maeneo yaliyokaribu na wakulima katika vifungashio tofauti vidogo tofauti na sasa mbolea ipo mifuko ya kilo 50.

"Tunaelekeza serikali kuanzia msimu ujao ilete mbolea kwenye vifungashio tofauti kilo 10, 25 na 50 ili mwananchi yeyote anunue kwa kiwango chenye uhitaji na si vinginevyo" anasema.

## Utofauti, umahiri kati ya kiongozi mwanaume na mwanamke kwenye kushughulikia mambo

**INATOKA UK.11**

bila ya kujali chama.Ni mwanamke hodari. Malumbano yapo katika mawazo na hii ndiyo demokrasia," anasema Shamim, akimwelezea Dk. Samia kama mwanamke anayefanya mambo mengi kwa manufaa ya makundi yote .

"Ni mwanamke shupavu, hana majivuno na mimi nasema mwaka 2025 tusimwache. Na ametuonyesha njia wanawake wengine kwamba tuthubutu. Elimu anayo, uwezo anao na ni mwanamke," anasema.

Anasema kwa utendaji wa Dk. Samia, hana wasiwasi kwamba mwaka 2025 'njia ni nyeupe' kwake kwa kuwa ameonyesha uwezo mkubwa.

Anasema serikali ya awamu ya sita imegusa sekta zote akitolea mfano wa afya, miundombinu, maji na nishati hivyo anawataka wanawake na wanaume wenye umri wa kushiriki uchaguzi wasimwache Rais Samia.

Mwanamke mbobevu wa Hisabati, Profesa Veridiana Masanja, anamwelezea Dk. Samia kama kiongozi wa mfano akitolea historia ya Chama Cha Demokraisa na Maendeleo (CHADEMA) namna ambavyo maandamano yake yalivyogharimu maisha ya wananchi.

Anasema maandamano yalizorotesha ustawi wa mambo mengi na kwamba awamu ya tano kuzuia mikutano ya hadhara ilileta butwaa kwa vyama vya upinzani jambo ambalo lilisababisha ufa kati ya wananchi na serikali.

Anatoa mfano kwamba jimbo la Arumeru Mashariki ambalo lilishikiliwa na upinzani liliathirika na maandamano ya CHADEMA na hawakupata maendeleo kutokana na chama hicho kususia vikao mbalimbali vya serikali.

"Nampongeza sana Rais Samia kwa kukubali mwaliko wa BAWACHA...hatuwezi kusema sisi ni nchi ya amani kama hatuko tayari kusikiliza reconciliation (maridhiano), hata ndugu wa tumbo moja huwa wanagombana lakini mazungumzo huwaleta pamoja," anasema.

Anasema alichokifanya Rais Samia ni hatua muhimu ambayo itaboresha mambo mengi nchini.

Mwisho.

VOLKANO YALIPUKA TLP

# 'Mzimu' wa Mrema unapokwamisha kuchagua wa kumrithi, mambo yakiahirishwa kiaina

## • Wafikishana kwa Msajili, lawama zamwangukia K/ Mkuu

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Tanzania Labour Party (TLP), kimekwama kumpata Mwenyekiti wa Taifa, baada ya uchaguzi kuahirishwa, katika mazingira tata na kusababisha wajumbe wa mkutano mkuu kuja juu.

Wakati hayo yanatokea, wagombea wa nafasi hiyo wamekimbilia kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, kutaka kujua hatma ya uchaguzi huo.

Machi 6, ilikuwa siku ya kufanya uchaguzi jijini Dar es Salaam ambapo wajumbe wote 142 wa mkutano mkuu, walikuwa wametua lakini wakiwa katika ofisi za makao makuu ya chama hicho, Magomeni Usalama, ghafla wakaambiwa zoezi limeahirishwa.

Tangazo la kuahirishwa kwa uchaguzi, lilitolewa na Katibu Mkuu, Richard Lyimo na kusababisha sintofahamu huku wajumbe wakihoji imekuwaje uchaguzi uahirishwe ghafla bila kuwapo maelezo ya kutosha.

Baada ya uchaguzi kuahirishwa katika mazingira hayo, wagombea wa nafasi hiyo, Aivan Maganza na wenzake Kananzaro Mwanga, Stanley Ndamugoba na Abuu Changawa, waliandika barua kwa Msajili.

Sehemu ya barua hiyo inasomeka; "Sisi wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa taifa wa TLP, tunaleta malalamiko yetu kwako kuhusu kuvunjwa kwa mkutano mkuu maalaum wa uchaguzi, kujaza nafasi ya mwenyekiti wa taifa wa chama, ambao ulikuwa ufanyike Jumatatu ya tarehe 6, Machi 2023, kwenye ukumbi wa Legho Hotel, kwa visingizio visivyo na ukweli wowote."

Maganza ambaye anawakilisha wagombea wenzake anasema barua ya kuvunja mkutano wa uchaguzi ilikuwa imesainiwa na Mwenyekiti na Katibu wa Bodi ya Wadhamini wa chama hicho.

Anafafanua katika barua hiyo kuwa bodi haina mamlaka ya kupinga maamuzi ya Halmashauri Kuu ya chama iliyokutana Mei 5 mwaka huu na kupitisha ya wagombea na kuamua uchaguzi ufanyike Machi 6 mwaka huu, ambapo ni kwa mujibu wa Katiba ya TLP ibara ya 18:5h(i) na kutaka maamuzi ya Halmashauri Kuu ya Taifa yaheshimiwe.

Barua hiyo inamalizia kwa kuelezea; "Hivyo tunakuomba Msajili wa Vyama vya Siasa uamuru uongozi wa TLP uitishe mkutano mkuu maalum haraka iwezekanavyo, ili demokrasia ndani ya chama itekelezwe."

### HOJA ZA MSAJILI

Msajili wa Vyama vya Siasa, baada ya kupokea malalamiko hayo, anaulima barua uongozi wa TLP a kiutaka ujieleze ni kwa nini uliahirisha uchaguzi wa Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho.

Barua hiyo ya Machi 9, mwaka huu yenye Kumbukumbu HA. 322/362A/38, ambayo imesainiwa na Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, inaelekezwa kwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Richard Lyimo, kuwasilisha maelezo katika ofisi hiyo.

Nyahoza anaeleza katika barua hiyo kuwa Ofisi ya Msajili, imepokea barua kutoka kwa baadhi ya wagombea wakilalamikia kuahirishwa kwa mkutano mkuu bila kufuata katiba na kanuni za chama hicho.

Aidha, barua hiyo inaendelea kueleza: "Kwa mujibu wa kifungu 5B cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258, uongozi wa TLP mnapaswa kuwasilisha maelezo kwa Msajili kujibu malalamiko ya wagombea hao." Barua hiyo inaeleza kuwa majibu ya uongozi wa TLP yatasaidia kumfanya Msajili wa Vyama vay Siasa kujua ukweli kuhusu sakata hilo.




Katibu Mkuu wa TLP, Richard Lyimo. **PICHA: MTANDAO**

> " Maganza ambaye anawakilisha wagombea wenzake anasema barua ya kuvunja mkutano wa uchaguzi ilikuwa imesainiwa na Mwenyekiti na Katibu wa Bodi ya Wadhamini wa chama hicho.

> " Wanachama, wapenzi pamoja na wajumbe wa halmashauri kuu, wajue kuwa haya ni mambo ya kisiasa yaliyo nje na uongozi, tunaahidi kuitisha tena uchaguzi kwa sababu wagombea...

Wakati barua ikielezea hayo, mmoja wa wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti Taifa, Mhandisi Aivan Maganza, anasema yeye na wenzake watatu waliaamua kuchukua hatua hizo ili kuhakikisha haki inatendeka.

Katibu Mkuu wa TLP, Richard Lyimo, ambaye alikuwa mgombea wa nafasi hiyo, akithibitisha kupokea barua hiyo na kufafanua kuwa atajibu kama alivyoelekezwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

### WANACHAMA WAFOKA

Mmoja wa wajumbe kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, Esta Mlay, analalamikia kitendo hicho na kudai kimeleta usumbufu na kutaka uongozi kuendelea na uchaguzi akisema ni aibu kwa chama chao kukaa muda mrefu bila mwenyekiti.

Katibu wa TLP Mkoa wa Dodoma, Damari Richard alisema kuahirishwa kwa uchaguzi huo kunatia shaka, kwa kuwa siku moja kabla walimaliza mkutano wao wa ndani kwa amani, lakini akashangaa kuona uchaguzi unaahirishwa.

"Hiki ni chama kikubwa, na sisi ni wajumbe kutoka miaka mbalimbali, tupo kwenye chama hiki kwa miaka mingi, lakini mambo kama haya yanatia aibu na tunapoteza imani kwa wafuasi wetu," anasema Damari.

### VIASHIRIA VYA RUSHWA

Wakati lawama zikielekezwa kwake, Katibu Mkuu Lyimo anadai kuwa kuahirishwa kwa uchaguzi huo kulitokana na kuwapo kwa viashiria vya rushwa kwa viongozi wanaowania nafasi hiyo.

Kulikuwa na shida kwa baadhi ya viongozi kwenye chama chetu, kwani tulishuhudia Naibu Katibu Mkuu, anatukanwa matusi ya nguoni na mmoja wa wagombea akimwambia yeye ni 'mwizi, mpumbavu na anakula rushwa mbele ya viongozi wa (TLP) Moshi, iliniuma sana," anasema Lyimo.

Lyimo ambaye pia ni mgombea wa nafasi hiyo, anasema baada ya kuahirisha uchaguzi huo, watakaa vikao vya ndani kupanga muda, kwa kuwa ni lazima wawe na mwenyekiti.

"Wanachama, wapenzi pamoja na wajumbe wa halmashauri kuu, wajue kuwa haya ni mambo ya kisiasa yaliyo nje na uongozi, tunaahidi kuitisha tena uchaguzi kwa sababu wagombea watakuwa walewale,"anasema.

Chama hicho kiko katika mchakato wa kufanya uchaguzi huo ili kujaza nafasi iliyoachwa na aliyekuwa mwenyekiti wa TLP Taifa, Augustine Mrema, ambaye alifariki dunia Agosti mwaka jana.

Nafasi hiyo kwa sasa inakaimiwa na Hamad Mkadam aliyechaguliwa na sekretarieti ya chama hicho Septemba mwaka jana, ikiwa ni wiki chache baada ya Mwenyekiti Mrema kufariki dunia.

BOLA AHMED TINUBU

# Ndiye rais ajaye Nigeria, kuapa Mei 29, ni bepari ila chanzo utajiri hakijulikani

•Ana msururu wa kashfa,kuuza 'unga', ufisadi na kesi Marekani





Viongozi wateule wa Nigeria, Rais Bola Tinubu na Makamu Kashimu Shettima. **PICHA: MTANDAO THIS DAY**

**Na Gaudensia Mngumi**

NI mfanyabiashara maarufu akimiliki kuanzia vyombo vya habari, usafiri wa anga hadi majengo ya kila aina, ndiye Bola Tinubu, rais mteule wa Nigeria.

Kwa sasa anajiandaa kula kiapo asubuhi ya Jumatatu Mei 29, katika Uwanja wa Eagle huko Abuja jiji kuu la Nigeria, kuwa rais wa taifa hilo.

Akiwa na miaka 70, yeye na mgombea mwenza Seneta Kashim Shettima wa jimbo la Daura, wameshinda urais wa taifa hilo lenye watu wengi zaidi barani Afrika kwa kura milioni 8.8, kwa mujibu wa matokeo ya mwisho ya uchaguzi, yaliyotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Nigeria (INEC).

Bola Tinubu, au 'political godfather' "mungu wa kisiasa" anasifika kwa umahiri wake,mikakati na ushujaa kwenye siasa, na kushinda kinyang'anyiro kikali cha kurithi Muhammadu Buhari kama rais wa Nigeria.

Ni nchi yenye watu zaidi ya milioni 120, lakini rais akishinda kwa kura milioni 8.8.

Tinubu anaelezwa kuwa hakuwahi kuficha azma yake ya kutaka kuwa rais wa Nigeria kwani bilionea huyo ambaye wengi humwita 'kikongwe' na kizee cha miaka 70 ametimiza lengo lake la maisha kwa kushinda urais wa taifa hilo japo kwa kura kiduchu milioni 8.8.

Licha ya maswali mengi kuhusu afya yake na madai ya ufisadi, kuuza dawa za kulevya, yaliyopita, gavana huyo wa mara mbili wa Lagos atamrithi Muhammadu Buhari, jenerali wa zamani wa jeshi, ambaye Tinubu anajisifu kuwa ndiye aliyesaidia kumuweka madarakani.

Tinubu anaangalia mbele, akiamini kuwa ushindi ni ushindi hata kwa goli la mkono, licha ya chama chake tawala cha All Progressives Congress (APC) kinakabiliwa na shutuma za udanganyifu katika uchaguzi uliofanyika Jumamosi Februari 25, 2023 kutoka kwa wapinzani wake wawili wakuu. Lakini maofisa wa uchaguzi na APC wametupilia mbali madai hayo.

**HAKUBALIKI NYUMBANI**

Mara nyingi Tinubu hujulikana kama chifu wa "Jagaban", Kwa Kiyoruba ambalo ni kabila kubwa la Nigeria, Jagaban ni jina au cheo anachopewa shujaa na jasiri, aidha ni mnyama asiyeogopa chochote!

Tinubu ametumia miaka mingi kujenga ngome yake kisiasa Lagos na kuunda mtandao wa kitaifa wa mawasiliano kutoka kwa vyama vya ushirika vya wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo na pia jumuiya za wasafirishaji hadi mashirika na taasisi za kisiasa akisaka kuungwa mkono.

Hata hivyo, ngome ya Lagos na wapambe aliodhani anao , katika matokeo yaliyoleta mshangao mgombea walimtosa. Mpinzani wake wa Chama cha Labour, Peter Obi, alimgaragaza kwenye jimbo la Lagos alilodhani ni ngome yake ya jadi.

"Unashinda baadhi ya maeneo,lakini unapoteza kwingine ," Tinubu anasema kuhusu matokeo hayo, akiwataka wafuasi wake kuwa watulivu na kujiandaa kwa ushirikiano.

Siku kadhaa baadaye, kiongozi huyo alifanya kampeni kwa kauli mbiu "Ni zamu yangu", alithibitishwa kuwa mshindi wa urais, licha ya kupata kura kiduchu, ambazo wagombea wawili Peter Obi wa Labour na Abubakar Atiku wa chama PDP walimzidi kwa mbali.

**ANAANZIA MAREKANI**

Tinubu aliyezaliwa miaka 70 iliyopita katika eneo la kusinimagharibi la Nigeria ni Myoruba, aliyesoma uhasibu nchini Marekani na alifanya kazi kwenye kampuni kadhaa za Amerika, ikiwa ni pamoja na mtunza hazina katika kampuni kubwa ya mafuta ya ExxonMobi.

Anaanza kuwa mwanaharakati wa kisiasa kabla ya kuwa seneta na baadaye gavana wa Jimbo la Lagos, ambalo analiongoza kutoka 1999 hadi 2007.

Wafuasi wa Tinubu wanaamini mafanikio ya Lagos yanayonekana leo ni kazi yake, wakitamba kuwa jimbo la jiji kubwa lenye uchumi bora zaidi nchini Nigeria haliwezi kusahau mchango wa Rais Mteule.

Hata hivyo, wakosoaji wengine wanasema hizo ni porojo za wafuasi waliochoka wa Tinubu, wakiamini kuwa mafanikio hayo ni kazi za siasa za ustawi wa Gavana Lateef Jakande, aliyeongoza jimbo hilo kuanzia 1979 hadi 1983, ambaye aliweka misingi ya Lagos ya leo.Jiji hilo lina watu milioni 21.

Akielezewa na washirika wake kama mwanamkakati mahiri wa kisiasa, alianzisha na kufadhili masuala ya kidemokrasia ambayo baadaye yalifanikisha kuundwa Action Congress of Nigeria, na kisha kufikia chama cha APC.

Anaelezwa kuwa na mchango mkubwa katika kuleta pamoja vikundi vya APC, na kumsukuma Buhari kushinda mwaka wa 2015 na kusaidia ushindi wa kumaliza miaka 16 madarakani kwa mpinzani wa People's Democratic Party (PDP).

Uchaguzi wa Buhari, ushindi wa kwanza wa upinzani nchini humo, pamoja na kuchaguliwa tena kwa 2019, ulichangiwa kwa sehemu kubwa na ushawishi wa kisiasa wa Tinubu, ambaye huenda amelipa fadhili kwa kumpigia debe kuwa mgombea na kisha kuwa rais mteule mwaka huu.

**TUHUMA ZA UFISADI**

Malumbano yanayomzunguka Tinubu wakati huu ni kuhusu shughuli zake za kifedha wakati akiwa madarakani kwenye jimbo la Lagos.

Anaaminika kuwa mmoja wa wanasiasa matajiri zaidi wa Nigeria na baada ya kuondoka madarakani anashutumiwa kwa ufisadi, utakatishaji fedha na kuendesha zaidi ya akaunti 12 za benki za kigeni.

Hata hivyo, hakuwahi kushtakiwa wala kuhojiwa na muda wote amekuwa akikanusha makosa wala tuhuma hizo.

**'MZUNGU WA UNGA'**

Katika kampeni, wakosoaji wa PDP walimtaja kama "mchafuko", mwoga na aliyeathiriwa na unga akijihusisha na dawa za kulevya", wakimaanisha wana wasiwasi na afya yake na pia wanazungumzia kesi ya mwaka 1993 katika mahakama ya Marekani ambayo ilitaifisha mali zake zinazohusiana na dawa za kulevya kutoka kwenye akaunti yake ya benki za Marekani

Chanzo cha utajiri wake hakijajulikana lakini ana maslahi katika ubia kadhaa wa kibiashara, kutoka vyombo vya habari na usafiri wa anga hadi ushauri wa kodi, hoteli na umiliki wa mali isiyohamishika ya ardhi na majengo.

Mkosoaji wake anamtaja kama "mwanasiasa mchoyo" ambaye amekusanya vyanzo vikuu vya mapato kutoka Lagos na kujitengenezea utajiri mkubwa akiwaacha hoi maskini.

***CHANZO: Al JAZEERA***



# Watumishi afya wakumbushwa kuzingatia maadili kwa wagonjwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekalaghe amewahimiza watumishi wa sekta ya afya hususani wauguzi kuzingatia maadili wanapotoa huduma kwa wagonjwa.

Aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano wa jukwaa la wauguzi na wakunga viongozi hapa nchini ulioandaliwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Alisema wauguzi na wakunga wanapaswa kuzingatia utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa kuwa ndiyo kipimo cha msingi kwa mteja.

"Kazi mnayofanya ni ibada hivyo ni muhimu sana kuzingatia na kujipima ubora wa huduma unayotoa , unaweza ukafanikiwa kwa vitu vingi sana kwa sababu wagonjwa unaowahudumia wanakuombea kwa mwenyezi Mungu, narudia kuwakumbusha ninyi ni Jeshi kubwa na mnaotoa taswira kubwa kwa sekta ya afya"alisema.

Kuhusu utoaji wa huduma, Dk. Shekalaghe aliwataka wauguzi na wakunga kutoa huduma kwa upendo kwa kuwa kuna matokeo makubwa katika sekta ya afya.

"Upendo unasaidia sana kujenga umoja kwani mgonjwa anapohitaji huduma hasaidiwi na mtoa huduma mmoja tu, hivyo ninyi mnapokuwa na upendo kati yenu lazima huduma inakuwa bora, na penye uongozi mzuri pana mabadiliko," alisema.

Muuguzi Mkuu wa Serikali, Ziada Sellah alisema mkutano huo utasaidia kuweka mikakati endelevu katika uboreshaji wa huduma za afya katika ngazi zote na kujifunza masuala mbalimbali, ikiwamo uongozi na kujadili kero zinazowakumba wauguzi.



Mwenyekiti wa kamati ya mazingira Wanawake na Samia mkoa wa Dodoma, Bhoke Mkami, akipanda mti kwenye eneo la Shule ya Msingi Chang'ombe, jijini Dodoma jana. Wa (tatu kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bil.2.3/- zaokolewa upandikizaji figo Hospitali Benjamin Mkapa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KWA miaka mitano serikali imeokoa Sh.bilioni 2.3 ambazo zingetumika kusafirisha wagonjwa wa figo nje ya nchi, tangu kuanza kutolewa kwa huduma ya upandikizaji figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH).

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa Habari akisema fedha hizo zimeokolewa kutokana na gharama nafuu ya upandikizaji figo hapa nchini inayotolewa na BMH.

Alisema huduma ya upandikizaji figo ilitolewa kwa wagonjwa 33 na kati ya hao 22 wamepandikizwa na wataalamu wa ndani ya nchi.

"Tunaishukuru Tokushukai Medical Group kwa kukubali kushirikiana na serikali kuanzisha huduma za upandikizaji figo hapa Benjamini Mkapa,"alisema Dk.Chandika.

Akielezea gharama za upandikizaji figo hapa nchini kwa mgonjwa mmoja, alisema ni Sh. milioni 35 ambazo hutumika kwa ajili ya maandalizi kuanzia vifaa tiba hadi dawa, tofauti na mgonjwa akipelekwa nje gharama yake inakuwa kati ya sh. milion 77 hadi 80.

Alisema ugonjwa huo unatakiwa mtu awe na fedha nyingi kuanzia usafishaji damu, ambayo ni hatua ya mwanzo kabla ya kufanya upandikizaji figo. Dk.Chandika alibainisha mgonjwa hutakiwa kusafisha damu walau mara tatu kwa wiki, ambayo hugharimu Sh.700,000 hadi 900,000.

Akielezea kuhusu wagonjwa waliotibiwa hospitalini hapo, alisema wote wanaendelea vizuri, hakuna aliyepata tatizo baada ya kufanyiwa upandikizaji.

"Nawashauri jamii wasisite kumtolea ndugu yake figo kama anauhitaji wa kiungo hiko, kwa sababu unayetoa na anayepewa wote mnakuwa salama kutokana na uchunguzi unaofanywa na jopo la madaktari bingwa,"alisema Dk. Chandika.

Kadhalika, Dk. Chandika alisema wanahitaji kuongeza wataalamu wa upandikizaji figo ili kuzidi kuongeza ujuzi wao.

Alisema kunahitajika wataalam wasiopungua 32 kwa upandikizaji mmoja.

Mwenyekiti wa Tokushukai Medical Group Dk. Higashiue Shinichi alisema taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na ili kuhakikisha Benjamin Mkapa inapiga hatua katika suala la upandikizaji figo kwa wagonjwa.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) Prof. Lughano Kusiluka, aliwapongeza BMH na Tokushukai Medical group kwa ushirikiano wanaoufanya, huku akisisitiza waendelee kuitangaza huduma hiyo kwa jamii.

## Sekta binafsi watakiwa kutengeneza fursa kwa vijana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imezitaka sekta binafsi kuwatengeneza fursa vijana hususani kwenye sekta ya kilimo ili wajikwamue kiuchumi.

Naibu Katibu Wizara ya Kilimo, Dk. Hussein Omary aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akifungua programu ya Building Better Tomorrow (BBT) kwa mashirika yasiyo ya kiserikali.

Alisema kuwa lengo la mkutano huo ni kuhakikisha utekelezaji wa programu hiyo Wizara ya Kilimo inashirikiana na wadau wote muhimu ili rasilimali zitumike kuwezesha vijana kushiriki katika kilimo.

Dk.Omary alisema BBT- YIA ni mpango wa nchi nzima ambao umekusudia kuwaunganisha vijana katika biashara moja ya kilimo itakayokuwa endelevu na yenye faida katika kila moja ya vijiji hapa nchini.

"Ninaomba sekta binafsi hakikisheni mnatengeneza fursa kwa vijana, hii itawasaidia kuwainua rika hilo kiuchumi,"alisema Dk. Omary.

Alisema kuwa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi 2022 yamebainisha kuwa zaidi ya asilimia 44 ya Watanzania ni vijana wenye umri kati ya miaka 18, hivyo uanzishaji wa maeneo maalumu kwa vijana waliopo katika kilimo biashara kutawasaidia kujiajiri wao wenyewe.

Aidha, alisema mashirika yasiyo ya kiserikali yana nafasi kubwa zaidi kusaidia kutengeneza fursa za vijana katika kilimo,

kuongeza kuwa wakifanya hivyo watasaidia kubadilisha mawazo hasi ya vijana kwenye kilimo biashara.

"Kuna vijana wengi hawana ajira licha ya kuwapo kwa fursa mbalimbali kwenye sekta ya kilimo, mashirika wanapaswa kutoa elimu ya mnyororo wa thamani kwenye kilimo ili kuwahamasisha vijana ikiwamo kuwabadilisha,"alisema Dk. Omary.

Alisema Tanzania ina NGO's zaidi ya 4,000 zinazojihusisha na sekta ya kilimo isipokuwa uwekezaji haujaweza kuratibiwa ipasavyo kutokana na kutokuwa na taarifa ya baadhi ya NGO's shughuli zinazofanyika.

Kutokana na hilo, aliwataka washiriki wa mkutano huo kujadili na kuona namna ya kuimarisha ushirikiano wa Wizara ya Kilimo na NGOs katika utekelezaji wa miradi ya kuwawezesha vijana na wanawake kufanya kilimo biashara chini ya programu ya BBT.

Mratibu wa BBT, Vumilia Zikankuba alisema kuwa mpango mkakati wa programu ni uanzishwaji wa maeneo maalum kwa ajili ya vijana waliopo katika kilimo biashara ili kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo kwa vijana.

Alisema maeneo yatakaanzishwa na mengine kuboreshwa kwenye miundombinu yatagawanywa katika mashamba ya vitalu.





# Afariki dunia madai kutaka kuiangamiza familia yake kwa moto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa eneo la Nyigamba, Kata ya Itezi jijini Mbeya, Hamis Pius (41) amefariki dunia baada ya kujifungia chumbani na mke wake kisha kuwasha moto kwa kutumia mafuta ya petroli.

Aidha, katika tukio hilo mke wa marehemu aitwaye Rebelia Makoso (38) pamoja na mtoto wao, Mkeshilisi Hamis (21) walijeruhiwa kwa kuungua na moto wakati wakipambana kujiokoa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga alisema tukio hilo lilitokea machi 8, mwaka huu usiku wakati wanandoa hao walipokuwa wamelala chumbani.

Kamanda Kuzaga alisema chanzo cha tukio hilo ni mgogoro wa ndoa uliokuwa unaendelea kufukuta baina ya wanandoa hao ambao hata hivyo hakuutaja kwamba ulikuwa unasababishwa na nini.

Kamanda Kuzaga alisema siku ya tukio Hamis alinunua mafuta ya petroli na kuyahifadhi ndani bila wanafamilia kujua na wakati wakiwa wamelala usiku, marehemu alifunga mlango na kuwasha moto kwa lengo la kuteketeza familia nzima. Alisema baada ya moto huo kulipuka mke wake alipiga kelele akiomba msaada kwa watoto ambao walikuwa wamelala chumba kingine.

Alisema baada ya kelele hizo kusikika, mtoto wao aitwaye Mkeshilisi alikwenda kutoa msaada lakini akakuta mlango umefungwa kwa ndani na ndipo alipoamua kuuvunja kwa kuupiga teke.

Alisema baada ya kuufungua mlango huo alimtoa mama yake nje na alipotaka kumtoa baba yake aligoma na baada ya kijana huyo kuona moto unamzidi alikimbia na ndipo umauti ulipomkuta baba yake.

"Kwahiyo kijana naye aliungua wakati akiendelea na harakati za kuwaokoa wawili hao, tunamshukuru Mungu kwamba wanafamilia wengine walipona maana inaonyesha lengo la mkuu huyo wa kaya ilikuwa kuteketeza familia nzima," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema majeruhi walikimbizwa katika Hospitali ya Igawilo kwa ajili ya matibabu, baadaye walihamishiwa katika Hospitali Teule ya Ifisi iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Alisema kwa sasa majeruhi hao wanaendelea vizuri na matibabu, huku uchunguzi zaidi wa tukio hilo ukiendelea ili kujua chanzo halisi cha uamuzi wa marehemu

Kamanda Kuzaga aliwataka wanafamilia kuacha kujichukulia sheria mkononi na kwamba wanapokuwa na migogoro ya ndoa wanatakiwa kutumia vyombo mbalimbali kusuluhisha migogoro hiyo.

Alisema migogoro ya ndoa inatakiwa kutatuliwa na viongozi wa serikali za mitaa ama dawati la jinsia na watoto ambalo lipo kwenye wilaya zote nchini.

Aidha, katika hatua nyingine Kamanda Kuzaga alisema Jeshi hilo linaendelea na operesheni kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo kwa lengo la kuwadhibiti wahalifu.

Alisema katika operesheni hizo Jeshi la Polisi limewakamata vijana mbalimbali wanaojihusisha na matukio ya uhalifu ikiwamo uuzaji wa dawa za kulevya aina ya bangi.



Mwalimu wa malezi na makuzi ya watoto, Dilawena Sichalwe akionyesha kwa vitendo namna ya kuwafundisha watoto wadogo wakati wa uzinduzi wa Programu Jumuishi ya Makuzi na Malezi ya watoto, katika Hospitali ya Aga Khan jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Serikali yapiga marufuku ununuzi maparachichi mabichi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI mkoani Mbeya imepiga marufuku wanunuzi wa maparachichi kununua matunda hayo kwa wakulima wilayani Rungwe yakiwa bado hayajakomaa kwa maelezo kuwa mbinu hiyo inatumika kuwanyonya wakulima.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alipiga marufuku hiyo juzi alipozungumza na wananchi wa maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo kuhusu maendeleo ya kilimo cha zao hilo.

Alisema kitendo hicho mbali na kuwanyonya wakulima pia kimekuwa kikishusha thamani ya matunda ya wakulima hao katika soko la kimataifa.

"Tayari nimeagiza vyombo vya ulinzi na usalama ya mkoa kuanza kufuatilia na watakaobainika watachukuliwa hatua ikiwemo kufutiwa leseni zao na mzigo kutaifishwa,"alisema Homera.

Aliwataka maofisa mbalimbali wa serikali wilayani humo kushiriki katika kudhibiti uhuni huo unaofanywa na wanunuzi huku akisisitiza kuwa watakaokamatwa wakinunua kupitia njia zisizokuwa rasmi watachukuliwa hatua.

Alisema serikali imekuwa ikitoa maelekezo ya mara kwa mara lakini utekelezaji umekuwa ukisuasua jambo ambalo linaweza kusababisha migogoro na wafanyabiashara hao.

Aidha, aliwaonya wakulima kuachana na tabia ya kuingia tamaa na kuuza kwa bei ya hasara na badala yake watoe ushirikiano kwa serikali kuwafichua wanunuzi wa kampuni na wafanyabiashara wakaidi.

# Ukosefu taulo za kike chanzo utoro kwa wanafunzi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

UKOSEFU wa taulo za kike na chumba cha kujisitiri wakati wa hedhi kwa wasichana wanaosoma Shule ya Sekondari Sangambi iliyopo katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imetajwa kuwa chanzo cha utoro kwa wanafunzi hao.

Aidha hali hiyo imetajwa kuwa ni miongoni mwa vyanzo vya kudorora kitaaluma kwa wanafunzi wa kike kutokana na kukosa masomo wakati wanapokuwa kwenye siku zao.

Mmoja wa walimu wa shule hiyo, Jackline Charles aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya utoaji wa taulo za kike kwa wasichana kwenye shule zote za sekondari katika wilaya hiyo.

Kampeni hiyo imeanzishwa na Veronica Masache ambaye ni mke wa Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka kwa lengo la kulisaidia kundi hilo kuendelea na masomo hata wanapokuwa kwenye hali hiyo.

Alisema katika shule hiyo wasichana 52 wamekatisha masomo kutokana na ukosefu wa taulo za kike jambo ambalo alisema limekuwa pia likiahatarisha afya za kundi hilo.

Alisema asilimia kubwa ya wanafunzi hao wamekuwa wakitumia vitambaa kujisitiri jambo ambalo huwa linawasababishia magonjwa ikiwamo fangasi na miwasho.

"Wanafuzi hawa huwa wanalazimika kukaa nyumbani wakati wanapokuwa kwenye siku zao, huwa wanapoteza kati ya siku tano mpaka saba kwa mwezi na hivyo kuwafanya wakose masomo kwa miezi mitatu kila mwaka," alisema Jackline.

Alimshukuru Veronica kwa kuanzisha kampeni hiyo kwa maelezo kuwa itasaidia kupunguza utoro kwa wasichana pamoja na kuwainua kitaaluma.

Akizungumza baada ya kuzindua kampeni hiyo na kugawa taulo hizo katika shule hiyo ya Sangambi, Velonica alisema kwa sasa teknolojia ya mawasiliano imekua kwa kiwango kikubwa hali inayosaidia kujua matatizo ya watu mapema.

Alisema kipindi hiki cha mabadiliko ya teknolojia kimeambatana na mabadiliko mengi na hivyo hata wasichana wanatakiwa kuendana na teknolojia hiyo kwa kuachana na vitambaa walivyokuwa wanavitumia kujisitili.

Alisema matumizi ya taulo hizo za kisasa ni salama kwa afya za wasichana tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo walikuwa wanaugua magonjwa kama fangasi na miwasho kutokana na kutumia vitambaa.

Aliwaka baadhi ya wazazi ambao wamekuwa wakiwashawishi watoto wao kuacha masomo ama kufanya vibaya kwenye mitihani ili waolewe kuacha tabia hiyo kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinawarudisha wanawake nyuma.

Aidha, aliwataka wasichana hao kuacha tabia ya kuchanganya masomo na mapenzi ili wafikie malengo yao ikiwa ni pamoja na kuwa viongozi wakubwa nchini.



# Wakazi Dunga wapewa fidia kupisha uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI 37 wa Kijiji cha Dunga Zuze Wilaya ya Kati Unguja wamelipwa fidia kupisha eneo hilo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda.

Akizungumza jana katika ulipaji fidia kwa wananchi hao, Waziri wa Biashara, Maendeleo na Viwanda, Omar Said Shaban alisema kuwa wizara yake imeidhinishiwa na Serikali ya Zanzibar, Sh. milioni 500.7 kwa ajili ya fidia za wananchi hao.

Alisema serikali imetenga eneo hilo lenye ukubwa wa hekta 173 kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda ili wananchi kupata maendeleo kupitia uwekezaji huo.

"Fidia hii inatokana na azma ya serikali ya kuendeleza sekta ya viwanda nchini ambapo tayari maeneo kadhaa yameshatengwa ikiwamo lile la Chamanangwe Kisiwani Pemba,"alisema.

Waziri huyo aliwapongeza wananchi walioathirika na uwekezaji wa eneo hilo kwa ushirikiano wao mwanzo hadi mwisho wa zoezi hilo, kwamba bila ya pingamizi wameridhia eneo hilo kwa shughuli ya uwekezaji wa viwanda.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ali Khamis, alisema awali eneo hilo wananchi walilitumia kwa shughuli mbalimbali ikiwamo za kilimo, lakini baada ya serikali kulichukua eneo hilo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda ilifanya tathmini ya ardhi hiyo na kulipa fidia hiyo.

Naibu Sheha wa Shehiya ya Dunga Kiembeni, Kesi Makame Mussa, alisema uwekezaji huo umepelekea kutambulika kwa Kijiji cha Dunga Zuze ambapo pia itatambulika zaidi baada ya lengo la serikali kukamilika la uwekezaji wa viwanda katika eneo hilo.

"Tumefikia hatua hadi sisi viongozi katika shehia tukaonekana kama wasaliti wa wananchi kwa upande wa serikali, lakini leo hii wananchi wametufarahia na wameanza kuona matunda kwa sababu kijiji hiki kilikuwa hakifikiki kwa sababu hakikuwa na miundombinu ya barabara," alisema.

Mmoja wa wananchi hao Mwanajuma Mussa Tenga aliishukuru serikali kwa fidia hiyo na kusema itasaidia katika kuendesha maisha yao baada ya kilimo chao kuathiriwa na uwekezaji huo.

Aidha, aliiomba serikali itakapokamilisha uwekezaji huo wa viwanda kutoa kipaumbele cha ajira kwa wananchi wa kijiji hicho ili vijana wao kufaidika na uwekezaji huo.

Mkazi mwingine Mwinyi Pembe Khamis, alisema katika mchakato huo wameshirikishwa kuanzia hatua za awali hadi kukamilika kwa fidia hiyo na hakuna malalamiko yaliojitokeza na kuridhia katika uwekezaji huo.

## Apendekeza kutolewa elimu kupinga udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKAGUZI wa Elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Maimuna Thabit, amesema kuna ulazima wa kutoa elimu ya udhalilishaji kwa watoto ili waweze kuwa na uelewa wa masuala hayo.

Aliyasema hayo jana katika sherehe maalum ya siku ya furaha, iliyoandaliwa na Shule ya True Vision Zanzibar kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) ofisi ya Zanzibar, ambayo iliwashirikisha watoto, wazazi, walezi na wanaharakati wa kutetea haki za makundi hayo.

Alisema Wizara ya Elimu inapiga vita vitendo hivyo kwa sababu wanafunzi wa kike na kiume ndiyo wanaofanyiwa vitendo hivyo.

Alisema vitendo vya udhalilishaji havipo shuleni bali hata baadhi ya wazazi ni wadhalilishaji kwa watoto wao na kuwasababishia maumivu.

Hivyo, aliwataka wazazi kuwa makini kwa watoto kuwa na mapenzi wakati wote kwa sababu watoto wanapodhalilishwa na wazazi hupoteza mapenzi.

"Kinababa wanatuvunja moyo sisi kinamama katika malezi ya watoto kwa sababu baadhi ya kinababa hawana ushirikiano katika malezi ya watoto na jukumu hilo humuachia mama pekee," alisema.

Alisema baadhi ya kinababa ndiyo chanzo cha udhalilishaji, jambo ambalo wanawake huathirika kuona mzazi mwezake anakuwa chanzo cha kuwadhalilisha watoto wao.

Ofisa kutoka TAMWA-Zanzibar, Zaina Salum Abdallah, alisema lengo la sherehe hizo ni kutoa elimu ya udhalilishaji hasa kwa watoto ili wafahamu viashiria ya vitendo hivyo.

Alisema watoto wanahitaji kulindwa na aina zote za udhalilishaji na kupewa haki zao za msingi ikiwamo haki ya elimu.

Nassor Haji ambaye ni mwanamtandao wa kupinga vitendo vya udhalilishaji, aliwataka wazazi kuwalinda watoto na vitendo vya udhalilishaji akisema vinaathiri nguvu ya taifa.

Aidha, alisema licha ya vitendo hivyo kuathiri taifa lakini humwathiri mtoto kisaikolojia, kimwili na wakati mwingine watoto wanaofanyiwa vitendo hivyo hushindwa kufanya vizuri katika masomo yao.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya DCB, Zawadia Nanyaro (kulia), akishikana mikono na baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtakuja, katika hafla ambayo DCB ilikabidhi msaada wa madawati 30 kwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge (hayupo pichani) ikiwa ni sehemu ya kampeni inayoendelea ya benki hiyo ya kusaidia elimu iitwayo 'Elimu Mpango Mzima na Mama Samia' shuleni hapo, Kunduchi, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara ya Afya yatoa hadhari uwapo matapeli kuhusu ajira

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya Zanzibar imetoa tahadhari kwa wananchi kuhusu kuwapo kwa baadhi ya taasisi zinazofanya vitendo vya utapeli kwamba wanatoa ajira katika sekta ya afya kwa kuajiri.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari na kusema madai ya utapeli ya ajira za afya yamesababisha usumbufu kwa wazazi na vijana wanaotafuta ajira.

Alisema utapeli huo unafanywa kwa kudai kati ya Sh. 500,000 hadi Sh. milioni moja, huku matapeli hao wakidai kwamba wanauwezo wa kutoa ajira za madaktari na wafanyakazi wengine wa sekta ya afya.

Mazrui alisema matapeli hao wanasema wana uhusiano na uhusiano wa Tume ya Utumishi Serikalini ambayo ndiyo inayohusika na mchakato wa ajira.

Alisema baadhi ya matapeli hao hujifanya wanatoka Wizara ya Afya kupitia Mkurugenzi wa Mipango na Utumishi na kumuhusisha kutangaza nafasi hizo.

"Napenda kuwajulisha wananchi ikiwamo wazazi kwamba kumejitokeza mitandao ya matapeli ambao hujipatia fedha kwa kudai kuwapo kwa nafasi za ajira katika Wizara ya Afya... suala hilo siyo kweli," alisema.

Waziri Mazrui alisema tayari suala hilo wamelifikisha kwa Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi zaidi na wahusika wake kuchukuliwa hatua za kisheria.

Katika hatua nyingine, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amefanya ziara katika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja kufuatilia utoaji wa huduma hospitalini hapo na kutembelea huduma zinazotolewa katika Idara ya Uchunguzi, Upasuaji, Kitengo cha Bima na Wagonjwa Wakulipia, pamoja na Idara ya Kinga.

Alisema serikali inaendeleza dhamira yake ya kuwapatia wananchi huduma ya afya bure ili kupata huduma hiyo ya msingi bila ya usumbufu wa aina yoyote.

## Hali ya utulivu yaanza kurejea Kivu

**KINSHASA,** DRC

NCHINI Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), hali ya utulivu imeshuhudiwa katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Masisi, hasa eneo la Sake jimboni Kivu Kaskazini, ambako tangu juma lililopita waasi wa M23 walikuwa wakishambuliana na wanajeshi wa serikali.

Utulivu umeripotiwa saa chache tangu kundi hilo litangaze kuondoka kwenye maeneo wanayoyadhibiti jana.

Mwenyekiti wa mashirika ya kiraia wilayani Rutshuru, Jean Bambaze, alisema "Waasi hao wamejiondoa katika maeneo ya Mweso na Karuba ila kwetu sisi tunaona ni kama ni ujanja wa hao M23."

Inaelezwa kuwa hayo yanajiri wakati makundi yenye silaha yakiripotiwa kuingia kwenye maeneo ambayo waasi wa M23 waliondoka.

Mkuu wa wajumbe na mwakilishi kutoka Ufaransa kwenye Umoja wa Mataifa, Nicolas de Rivière, mbali na kulaani uvamizi wa Rwanda dhidi ya DRC alikumbusha jukumu la kila mmoja katika mzozo huo, huku akieleza kuwa suala la kupiga vita makundi ya waasi kama M23, ni jukumu la FARDC.

Mkuu wa diplomasia ya Kongo Christophe Lutundula, alisema matamshi haya ni ya kashfa na hayakubaliki.

"Ni kosa kubwa kufikiria kuwa viongozi wa sasa wa nchi hii wanafikiria kwamba kuna nchi duniani itatatua matatizo ya raia wa Kongo hilo halikubaliki," alisema Lutundula.

**RFI**

**Mkuu wa wajumbe na mwakilishi kutoka Ufaransa kwenye Umoja wa Mataifa, Nicolas de Rivière, mbali na kulaani uvamizi wa Rwanda dhidi ya DRC alikumbusha jukumu la kila mmoja katika mzozo huo, huku akieleza kuwa suala la kupiga vita makundi ya waasi kama M23, ni jukumu la FARDC.**

# Kimbunga Freddy chaua takribani 100

**LILONGWE,** MALAWI

MAMLAKA ya kusini mwa Afrika zimesema kimbunga Freddy kilichoambatana na upepe mkali na mvua kubwa, kimerejea nchini Malawi na Msumbiji na kuua watu 100.

Kimbunga Freddy, kinachoelekea kuwa dhoruba ya muda mrefu iliyovunja rekodi ya kudumu, kilipiga sehemu za kusini mwa Afrika mwishoni mwa wiki iliyopita kwa mara ya pili ndani ya wiki chache, na kurejea tena baada ya mara ya kwanza kupiga katika eneo hilo mwishoni mwa mwezi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Msalaba Mwekundu zaidi ya miili ya watu 60 ilipatikana mchana katika eneo la kusini mwa Malawi ambako mvua kubwa ilisababisha mafuriko.

"Watu 100 wamefariki nchini Malawi, 93 wamejeruhiwa na watu 16 hawajulikani walipo kutokana na Kimbunga cha Tropiki cha Freddy," shirika la misaada ya kibinadamu, ambalo linasaidia katika shughuli za uokoaji na utafutaji, liliandika kwenye Twitter.

Pia inaelezwa kuwa kiwango kamili cha uharibifu na vifo nchini Msumbiji bado hakijabainika, kwani umeme na mawimbi ya simu yalikatika katika baadhi ya maeneo ya eneo lililoathiriwa.

Rais wa nchi hiyo, Lazarus Chakwera, alitangaza hali ya hatari katika eneo la kusini mwa nchi nchi hiyo baada ya kuelezea wasiwasi mkubwa kuhusu uharibifu uliosababishwa na kimbunga Freddy.

Msemaji wa Polisi wa eneo hilo Beatrice Mikuwa, alisema takriban miili ya watu 36 ilipatikana katika kitongoji kimoja cha Chilobwe, mjini Blantyre na kwamba mji huo uliathirika zaidi, huku dazeni za nyumba zikiwa zimesombwa na maji.

Pia inaelezwa kuwa Malawi iliamuru shule katika wilaya kumi za kusini kuendelea kufungwa hadi leo, huku mvua na upepo ukitarajiwa kuendelea kulikumba eneo la kusini mwa taifa hilo.

Shirika la ndege la Malawi, lilisema safari zote za ndege kwenda Blantyre zimefutwa mpaka itakapo tangazwa tena.

Aidha, hatua hiyo inafuatia ndege iliyokuwa ikielekea katika uwanja wa ndege wa Blantyre kukumbana na hali mbaya ya hewa katikati ya safari na kulazimika kurudi katika mji mkuu Lilongwe.

Idadi ya vifo ilitarajiwa kuongezeka, wakati mamlaka zilifanya jitihada za kuyafikia maeneo yote yaliyoathiriwa.

Malawi ndio nchi iliyoathirika zaidi na kimbunga hicho, ambapo hadi sasa watu 99 wamepoteza maisha yao kufuatia maporomoko ya udongo yaliyosomba nyumba kadhaa nchini humo.

Shirika la Umoja wa Mataifa la kushughulikia watoto UNICEF limetahadharisha kuwa, hali mbaya ya hewa kama hiyo iliyosababisha kimbunga, inaweza kuzidisha kuenea kwa magonjwa yatokanayo na maji chafu au kwa kunywa maji yasio salama kama vile kipindupindu.

Jumla ya waliouawa na kimbunga Freddy huko Msumbiji, Malawi na Madagascar tangu ilipotua kwa mara ya kwanza mwezi uliopita sasa ni takriban 136.

**VOA**



Barabara iliyoharibika kutokana na mafuriko ya mvua iliyoambatana na kimbunga Freddy huko Blantyre nchini Malawi juzi. **PICHA: AFP**

## Marekani, Uingereza na Australia kuanzisha manowari za nyuklia

**WASHINGTONG,** MAREKANI

MAREKANI, Uingereza na Australia zimefichua maelezo ya mradi wa pamoja unaolenga kuunda kundi jipya la manowari zinazotumia nguvu za nyuklia, ili kukabiliana na ongezeko la ushawishi wa China katika eneo la Bahari za Hindi na Pasifiki.

Chini ya makubaliano ya Okus, Australia itapata manowari ya kwanza kati ya tatu zinazotumia nguvu za nyuklia kutoka Marekani.

Washirika hao pia wanafanyia kazi kuunda kundi jipya la meli ambalo litatumia teknolojia za kisasa zaidi, ikiwa ni pamoja na vinu vya Rolls-Royce vinavyotengenezwa Uingereza.

China ilishutumu mradi huo mkubwa wa ushirikiano, ikionya kwamba makubaliano hayo yanawakilisha njia mbaya na hatari.

Ujumbe wa China kwa Umoja wa Mataifa (UN) pia ulishutumu washirika wa magharibi kwa kutatiza juhudi za kuzuia kuenea kwa silaha za nyuklia.

Beijing hapo awali ilitoa wito kwa nchi hizo tatu, kabla ya tangazo la mwanzoni mwa wiki, kuachana na mawazo ya vita baridi na michezo ambayo haileti matokeo.

Aidha, inaelezwa kuwa Russia nayo ililaani mkataba huo, ikisema kwamba utasababisha makubaliano ambayo yatadumu kwa miaka barani Asia.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergey Lavrov, alisema "Ulimwengu wa Anglo-Saxon unajenga mikataba kama vile Okus, kuendeleza miundombinu ya NATO barani Asia, na kucheza kamari katika makabiliano ambayo yatadumu kwa miaka mingi."

Pia Shirika la Kimataifa la Nishati ya Atomiki lilionya kuhusu hatari ya kuenea kwa nyuklia kutokana na mradi wa manowari unaoendeshwa na nyuklia uliozinduliwa na Marekani, Australia na Uingereza.

Hata hivyo, Rais wa Marekani Joe Biden, alisema kuwa mkataba huo unalenga kukuza amani katika eneo hilo, na kusisitiza kuwa manowari hizo zitakuwa zinaendesha nishati ya nyuklia na sio silaha za nyuklia.

Akizungumza pamoja na mawaziri wakuu wa Uingereza na Australia, Rishi Sunak na Anthony Albanese, mjini San Diego, California, Biden alisema makubaliano hayo hayatahatarisha dhamira ya Australia ya kuwa nchi isiyo na silaha za nyuklia.

**BBC**

## HABARI MICHEZO

# KATWILA ATOA SIRI YA USHINDI, ONGALA AWATAJA WACHEZAJI

**Saada Akida na Hadija Mngwai**

WAKATI Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, akisema nidhamu na kuwaheshimu Azam FC ni sababu kubwa ya wao kupata ushindi wa bao 1-0 juzi, Kocha Msaidizi wa 'Wanalambalamba' hao, Kali Ongala, amefunguka kuwa nyota wake wamekuwa wakicheza chini ya kiwango katika michezo ya ugenini jambo ambalo anahitaji kulifanyia kazi.

Ihefu juzi ilitumia vema uwanja wake wa nyumbani kwa kuibuka na alama tatu katika dimba la Highland Estates, Mbarali mkoani Mbeya bao pekee likifungwa na Raphael Daudi akiunganisha mpira wa faulo kutoka kwa Never Tigere.

Akizungumza na mwandishi wetu, Katwila alisema mchezo unakuwa mgumu unapocheza na timu aina kama ya Azam FC, lakini kucheza kwao kwa nidhamu kwa kuheshimu mpinzani wao kumewasaidia kufanikiwa kuvuna pointi tatu muhimu.

"Tumefanikiwa mipango yetu ya kuzuia pointi tatu nyumbani, niwapongeze wachezaji wangu kufuata maelekezo yote na kutumia vema mipira ya faulo na kupata bao 1-0.

"Tunao wachezaji maalum wa kupiga mipira ya faulo akiwamo Tigere (Never), ukiangalia hata mechi yetu dhidi ya Yanga, bao lilipatikana kwa mipira hiyo ya faulo, ilipigwa na nyota huyo lakini pia tuna wachezaji watatu wa kupiga mipira hiyo," alisema Katwila.

Kwa upande wa Azam FC, Ongalla alifunguka kuwa nyota wake wamekuwa wakicheza chini ya kiwango katika michezo ya ugenini jambo ambalo sasa anapaswa kulivalia njuga. Akizungumza na Nipashe, Ongali alisema katika mchezo wa juzi dhidi ya Ihefu wachezaji hawakucheza katika kiwango kinachostahili, hivyo hawakustahili kushinda mchezo huo.

"Makosa yamekuwa yakijirudia, inabidi tujitafakari ili tuweze kuelewa tatizo lipo wapi, sizani kama tulitakiwa kupoteza na vilevile tulikuwa hatustahili kushinda hii mechi kwa sababu timu imecheza chini ya kiwango kama tunavyojua timu yetu inavyocheza.

"Hivyo tunahitaji kuangalia jinsi tunavyoweza kujiimarisha sana sana mechi za nje ya nyumbani, makosa yamekuwa yakijirudia na si kitu kimoja, saikolojia yetu na namna tunavyoukabili mchezo kwenye hizi mechi, inabidi tuviangalie ili visijirudie katika mechi zinazofuata," alisema Ongala.




Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezi. Jumamosi timu hiyo itaikaribisha Horoya AC Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwenye mechi ya Kundi C ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA**

# Kocha Namungo alia na mabao ya krosi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi, amesema timu yake imekuwa ikiruhusu mabao mengi ya krosi, hivyo ana kazi ya kufanya kwenye uwanja wa mazoezi ili kuondoa hali hiyo.

Akizungumzia maendeleo ya timu yake ambayo Jumamosi iliyopita ilikumbana na kipigo cha mabao 3-2 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, Kitambi alitolea mfamo mechi hiyo akidai mabao ya krosi ndiyo yaliyowaua.

"Kwanza kabisa kwenye mechi dhidi ya Prisons, tangu nijiunge na Namungo sijawahi kuona timu yangu inacheza kipindi cha kwanza kibovu kama kile, tunawaacha watu wanakimbia bila kuwakaba, goli la kwanza inapigwa krosi, tunashindwa kumkaba mtu, wanafunga, inabidi turudi kwenye uwanja wa mazoezi kuyafanyia kazi kwa sababu mabao ya krosi ndiyo yanayotuua sana kwenye timu yetu," alisema kocha huyo.

Kitambi aliwaomba radhi mashabiki wa Namungo ambao walikuwa wamejazana kwenye uwanja huo wa nyumbani kuishangilia timu yao, lakini wakaambulia kipigo.

"Niombe msamaha kwa mashabiki, walikuja kwa wingi, lakini kiwango chetu kipindi cha kwanza hakikuridhisha kabisa, na hapa tulipo tuna deni kwao, kwa sababu walijazana sana, lakini hatukuwapa kile walichostahili," alisema kocha huyo.

Kwenye mechi hiyo mabao ya Prisons yalifungwa na Samson Mbangula dakika ya 14, Nurdin Chona dakika ya 29 na Jeremiaha Juma dakika ya 52, huku ya Namungo yakitumbukizwa nyavuni na Hassan Kabunda dakika ya 78 na Reliants Lusajo dakika ya 87.

Namungo inakamata nafasi saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi zake 32 na matokeo hayo yakaipandisha Prisons hadi nafasi ya 13 kwa pointi 25.

## Yanga Princess yapania ushindi leo

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Sebastian Nkoma, amesema timu yake ipo imara na tayari kuvaana na Mkwawa Queens katika mechi yao ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara itakayochezwa leo mkoani Iringa.

Yanga Princess itashuka uwanjani ikiwa na rekodi mbaya ya kupoteza mchezo wake uliopita ambao walikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Fountain Gate kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Kocha huyo wa zamani wa Simba Queens, alisema licha ya kupoteza mchezo huo hajakata tamaa kwani malengo yao ni kupata pointi tatu.

"Malengo yetu ni kupata pointi tatu kwenye mchezo huo, nimefanyia marekebisho makosa ambayo niliyaona kwenye mchezo wetu uliopita," alisema Nkoma.

Alisema wachezaji wake wana morali ya juu na kila mmoja ameahidi kufanya vema kwani wanatarajia kushika nafasi za juu kwenye msimamo wa ligi hiyo msimu huu.

"Mchezo uliopita hatukupata matokeo mazuri, tunaamini hakuna kinachoshindikana kama tutaendelea kushikamana," alisema Nkoma.

## Uchaguzi Chabata Aprili jijini Dodoma

**Na Shufaa Lyimo**

UCHAGUZI Mkuu wa Chama cha Baiskeli Tanzania (Chabata), unatarajiwa kufanyika Aprili 2, mwaka huu jijini Dodoma, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Najaha Bakari, aliwataka wadau mbalimbali wa mchezo huo kujitokeza kuchukuwa fomu za kuwania uongozi ndani ya chama hicho.

"Fomu zinapatika hapa BMT kila Mtanzania ambaye anajua amekidhi vigezo aje kuchukua kwani lengo letu ni kuhakikisha vyama vyote vya michezo vinaendelea," alisema Bakari.

Alisema nafasi zinazowaniwa ni mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu mkuu, katibu mkuu msaidizi pamoja wajumbe watano wa kamati ya utendaji.

Aidha, Bakari alisema usaili wa wagombea utafanyika April Mosi, mwaka huu mkoani humo hivyo kuwataka wagombea wote kufuata kanuni na taratibu za uchaguzi huo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED YAKOMAA NA KANE

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, kuelekea msimu wa majira ya joto. ***(ESPN)***

### NKUNKU SAFI CHELSEA

Christopher Nkunku atakuwa mchezaji wa Chelsea msimu ujao baada ya 'The Blues' hao kufikia makubaliano kamili na RB Leipzig kumsajili mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### SPURS YAMTAKA MARTINEZ

KLABU ya Tottenham Hotspur ina nia ya kumnunua Emiliano Martinez wa Aston Villa na wanaweza kuwasilisha ofa kwa mlinda mlango huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 30, wiki zijazo. ***(TyC Sports)***

### TEBAS AMTAJA MBAPPE

RAIS wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier Tebas, amesema anataka kumuona mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, akiichezea Real Madrid. ***(Sport)***

### JUDE AKUTANA NA MADRID

MWAKILISHI wa Real Madrid hivi majuzi alizuru Ujerumani kukutana na Jude Bellingham na familia yake baada ya kumfanya kiungo huyo wa kati wa Borussia Dortmund na England mwenye umri wa kati wa miaka 19, kuwa shabaha yao ya kwanza msimu ujao wa majira ya joto. ***(AS)***

### 'NEYMAR HAONDOKI PSG'

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar, mwenye umri wa miaka 31, hatarajii kuondoka PSG kwa vile anataka kumaliza soka lake na klabu hiyo ya Ufaransa. ***(Athletic)***

### DUMFRIES ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inaweza kufanya uhamisho mwingine msimu huu wa majira ya joto kwa mmoja wa walengwa wao wa muda mrefu, beki wa Inter Milan na Uholanzi, Denzel Dumfries, 26. ***(Football Insider)***

### KROOS KUBAKI MADRID

KIUNGO wa kati wa zamani wa Ujerumani, Toni Kroos, mwenye umri wa miaka 33, ameamua kusalia Real Madrid kwa walau msimu mmoja. ***(Mundo Deportivo)***

### ZAHA OFA NONO SAUDIA

WINGA wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 30, Wilfried Zaha, ambaye mkataba na Klabu ya Crystal Palace unamalizika msimu huu wa majira ya joto, amepewa ofa ya pauni milioni tisa kwa msimu na Klabu ya Al-Ittihad ya Saudi Arabia. ***(Mail)***

### SARA AMULIKWA WEST HAM

KLABU ya West Ham iko tayari kumenyana na RB Leipzig na Atletico Madrid kupata saini ya kiungo wa kati wa Norwich City, Mbrazil Gabriel Sara, mwenye umri wa miaka 23, msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### PELLISTRI SASA KUACHWA

MANCHESTER United pia wanapanga kumwacha winga wa Uruguay, Facundo Pellistri, mwenye umri wa miaka 21, kwenda nje kwa mkopo msimu ujao. ***(Evening sports Manchester)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MADRID YATENGA EURO MIL. 300 KWA BELLINGHAM

Katika dau hilo pia yumo Kvaratskhelia wa Napoli na Cancelo wa Man City hii ni baada ya...

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid wameripotiwa kuwatambua Khvicha Kvaratskhelia wa Napoli, Jude Bellingham wa Borussia Dortmund na Joao Cancelo wa Manchester City kama walengwa wao watatu katika mpango wa usajili wa euro milioni 300 kipindi cha majira ya joto.

Miamba hao wa Hispania wamekuwa wakimfuatilia Bellingham mwenye umri wa miaka 19, kwa miezi kadhaa, huku Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 22, akiibuka kuwa mmoja wa wanaotarajiwa kuibuka katika soka la dunia katika msimu wake wa kwanza kule Serie A.

Mustakabali wa Cancelo na pale City pia hauonekani baada ya Pep Guardiola kumruhusu akopeshwe kwa Bayern Munich, huku klabu hiyo ya Ujerumani ikisita kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu.

Wanaweza kuwa majina matatu makubwa zaidi kuhama katika dirisha lijalo la usajili, na Madrid wanasemekana kutaka kuwaleta wote kwenye LaLiga badala ya kuanza tena kumsaka Kylian Mbappe wa Paris Saint-Germain.

Kwa mujibu wa Fichajes.net, Madrid itajaribu kupata walengwa wote watatu wa juu kwa ada ya pamoja ya euro milioni 300.

Ripoti hiyo inasema wameridhishwa na bei ya Kvaratskhelia, ambayo inasemekana kuwa kima cha chini cha euro milioni 100, huku wakitarajia Liverpool kushindana nao katika mbio za euro milioni 150 kwa Bellingham.

Cancelo ana kipengele cha kununuliwa cha euro milioni 70 katika mkataba wake wa mkopo, ambao unasemekana kuwa mzuri zaidi kwa Madrid kuliko Bayern, kwani wanamwona kama suluhu ya muda mrefu kwenye beki ya kulia.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,090,5

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 2.34
X | 3.52
2 | 2.65

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA AIPA UBINGWA ARSENAL



**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema kusubiri kwa muda mrefu kwa Arsenal kutwaa taji la Ligi ya England kunawasaidia kuwa na morali na anawapa nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa huo.

Ushindi wa mabao 3-0 wa Arsenal dhidi ya Fulham Jumapili ulimaanisha kurejesha uongozi wao wa pointi tano dhidi ya City walio nafasi ya pili wakiwa na mechi 11 za kucheza.

Ushindi huo ulikuwa wa kawaida zaidi ukilinganisha na ule wa wiki iliyopita wa mabao 3-2 dhidi ya Bournemouth ambapo Reiss Nelson alifunga bao la ushindi dakika ya 97.

Guardiola alisema ukame wa muda mrefu wa Arsenal wa kunyakua taji la Ligi Kuu ambao hawajapata heshima hiyo tangu msimu wa 2003-04, umekuwa kichocheo cha wao kuupigania.

"Wana miaka mingi bila kushinda Ligi ya England na hiyo inakupa ziada kidogo kushinda mechi katika dakika ya 93, 96, 98. Hicho ni kitu ambacho hatuna kwa sababu tumeshinda mfululizo," alisema Guardiola akinukuliwa na BBC Sport.

Lakini Guardiola alisisitiza kwamba Arsenal ndio wenye nafasi kubwa zaidi, hata baada ya City kuwalaza 3-1 kwenye Uwanja wa Emirates.

# Havertz: Kiwango duni kimeleta shida

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Kai Havertz, anafurahia kiwango kizuri kwa mara nyingine tena, lakini alifichua kwamba alikuwa na matatizo ya kutokuwa kwenye kiwango yeye na wenzake.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ujerumani, ameanza mechi 22 kati ya 26 za Ligi Kuu England msimu huu.

Akiwa kwenye msimu uliojaa shinikizo huku kocha Graham Potter akipigania kazi yake, sasa Havertz anaona mwanga mpya.

Baada ya mabao nane na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 29 za ligi msimu uliopita, Havertz amefikisha mabao sita na asisti moja wakati huu.

Lakini alikuwa na bao moja pekee katika mechi 10 zilizopita kabla ya kufunga bao dhidi ya Leicester City Jumamosi kwenye mchezo walioshinda mabao 3-1.



Havertz alisema; "Soka ni maisha yetu, ukipoteza mchezo, bila shaka huna maisha rahisi pia na nadhani kila mtu nyumbani, haswa mpenzi wangu, amekuwa na wiki ngumu pia katika wiki na miezi iliyopita. Nadhani anafurahi sasa tena na mimi pia."

"Soka ni mchezo ambao tuna shinikizo nyingi. Tunataka kuwafurahisha mashabiki na ikiwa hautawafurahisha basi huna wakati mzuri."

Mchezaji huyo amesema kuwa itachukua muda kidogo kuwa kwenye ubora wake ingawa sasa anaona mambo yameanza kubadilika.

583,531/-

# MREMI ASEMA SIMBA CHANZO KUSHINDA MIL. 11/- SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Tabata Liwiti, Charles Ndechihiko Mremi, amejishindia kitita cha Sh. 11,555,580, ikiwa ni Bonus ya Jackpot ya SportPesa baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 alizocheza.

Akizungumza katika Ofisi za SportPesa Oysterbay, Dar es Salaam jana, Mremi alisema alianza kucheza na SportPesa kuanzia mwaka 2020, baada ya kuona jina la kampuni hiyo katika jezi za Simba ambayo ni shabiki mkubwa wa timu hiyo.

"Mimi nilianza kucheza SportPesa mwaka 2020, nilikuwa nanunua jezi kila zilivyokuwa zinatoka kila msimu. Kwa miaka ile Simba ilikuwa vizuri sana na kila nilipokuwa nikinunua jezi nilikuwa nakutana na jina la SportPesa.

"Nilipofuatilia niligundua kumbe hii ni kampuni ya kubashiri na kujua kwa undani wanafanyaje fanyaje kwenye biashara yao," alisema.

Charles anaendelea kusema wakati ameanza kucheza miaka miwili iliyopita alikuwa anashinda Sh. 11,000, laki mbili, laki tatu na nyingine ndogo ndogo, ambazo zilimpa moyo wa kendelea kubashiri kila alipopata nafasi.

Kuhusu mkeka huo wa Jackpot alioshinda, Mremi alisema aliziona mechi za Jackpot Jumatatu iliyopita na kuweka mkeka wake siku hiyo hiyo, baada ya kupitia kwa kuangalia historia ya timu, magoli waliyofunga na pointi walizonazo katika msimamo wa ligi.

"Naweza kusema Mungu ni mwema sana kwangu, kwani kwanza, nilishinda mkeka wakati nikiwa ninaumwa na nimetoka hospitali. Charles anasema yeye ana kawaida ya kila Jumatatu na Alhamisi au Ijumaa kuweka mikeka ya Jackpot za SportPesa.

Mimi nina kawaida ya kuweka japo 2000 au 3000 kwenye simu yangu na kisha kucheza Jackpot za SportPesa ambazo moja huchezwa katikati ya wiki na nyingine mwishoni mwa wiki.

"Katika mkeka wangu huu ulioshinda nilicheza majira ya saa sita mchana. Kawaida huwa sina muda wa kufuatilia matokeo ya mechi nilizocheza, mpaka zikiisha ndio nasubiri kuona sms kama nimeshinda au la. Sasa kwa mkeka huu ilikuja sms ya hongera lakini kwa muda ambao sms inaingia nilikuwa sebuleni kwangu nimepumzika naangalia muvi, baada ya kutoka hospitali.

"Sikutumia simu yangu kwa muda, lakini sms ya hongera ilikuwa tayari imeshaingia. Baadaye kidogo nilipigiwa simu na mtoa huduma nikiulizwa kama nimeona sms. Kwa kuwa nilikuwa ninaumwa sikutilia maanani na nikajibu sijaona sms wanayoniambia, baada ya muda kidogo nilijaribisha kuwasiliana na namba iliyonipigia kwa kufanya kama natuma Tigo Pesa. Zoezi hilo halikufanikiwa hivyo ikanipa hisia labda ni matapeli wanajaribu kunichezea akili wanipige hela," alisema na kuongeza.

"Nilikumbuka kwamba nina jamaa yangu Juma Pembe.

Juma anashiriki sana kwenye kubeti. nilimwelezea kilichojiri na yeye akashauri tutafute kwenye mtandao (google) ofisi za SportPesa zilipo kisha tundwe, ilipotimu asubuhi, Juma alinitumia ramani na nikaifuatisha mpaka kufika. Kwa kweli nimefurahi sana kwa kuwa tangu nimefika nimepokelewa vizuri na kupitishwa katika hatua mbali mbali za uhakiki za kiofisi na sasa nimetoka kukabidhiwa hundi ya pesa niliyoshinda.'

Akizungumzia fedha hizo ataifanya nini, alisema kitu cha kwanza atafanya ni kufungua na kuwawekea kiasi cha fedha watoto wake wawili ambao bado ni wadogo sana.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Kampuni ya SportPesa, Sabrina Msuya, alimpongeza Mremi kwa ushindi wake na kumtaka aendelee kucheza kwani bado Jackpot kila wiki inazidi kuongezeka.




Mshindi wa Jackpot Bonus, Charles Mremi kutoka Tabata, Dar es Salaam, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 11.5 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Yanga yaiandalia dozi kali Monastir

INATOKA UK. 24

hiyo.

"Tutakuwa na mazoezi ya aina mbili, asubuhi tunafanya gym na jioni uwanjani, hii mechi ni ngumu sana maana tumeona jinsi tulivyocheza mechi ya kwanza, mapungufu yaliyojitokeza tunayafanyia kazi kuelekea mechi yetu ijayo.

"Kuna wachezaji wanakosa mwendelezo, leo wanacheza vizuri mechi inayofuata wanaonesha kiwango cha chini hilo sifurahishwi nalo, kitu ambacho kwa sasa nakifanyia kazi," alisema Nabi.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.18/03/23 | 18:00 | Aberdeen FC vs Heart of Midlothian FC | 2.38 | 3.40 | 2.65 |
| 02.18/03/23 | 18:00 | Rotherham United vs Cardiff City | 2.55 | 3.15 | 2.65 |
| 03.18/03/23 | 18:00 | Stoke City vs Norwich City | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 04.18/03/23 | 18:15 | Albacete Balompie vs Granada CF | 2.55 | 2.95 | 2.80 |
| 05.18/03/23 | 18:30 | Portimonense SC vs FC Vizela | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 06.18/03/23 | 20:30 | Espanyol Barcelona vs RC Celta de Vigo | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 07.18/03/23 | 20:45 | FC Emmen vs Sparta Rotterdam | 2.50 | 3.10 | 2.70 |
| 08.18/03/23 | 21:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs FC Metz | 2.60 | 2.95 | 2.75 |
| 09.18/03/23 | 21:00 | Chamois Niort FC vs Stade Lavallois MFC | 2.60 | 3.00 | 2.70 |
| 10.19/03/23 | 14:15 | FC Groningen vs SC Heerenveen | 2.70 | 3.20 | 2.46 |
| 11.19/03/23 | 14:30 | Sampdoria Genoa vs Hellas Verona | 2.85 | 3.00 | 2.48 |
| 12.19/03/23 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Hannover 96 | 2.46 | 3.30 | 2.65 |
| 13.19/03/23 | 16:30 | Excelsior Rotterdam vs SC Cambuur | 2.55 | 3.30 | 2.50 |
| 14.19/03/23 | 17:00 | ESTAC Troyes vs Stade Brest 29 | 2.70 | 3.20 | 2.45 |
| 15.19/03/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Villarreal CF | 2.90 | 3.05 | 2.40 |
| 16.19/03/23 | 19:00 | FK Austria Wien vs SK Rapid Wien | 2.40 | 3.15 | 2.45 |
| 17.19/03/23 | 20:00 | Lazio Rome vs AS Roma | 2.60 | 2.95 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 15/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 1945 | Maktaaral vs Atyrau | 2.12 | 3.08 | 3.19 |
| 13:00 | 3135 | Iraq vs Japan U20 | 6.64 | 3.63 | 1.48 |
| 14:30 | 5745 | Ranong United vs Chainat FC | 2.76 | 2.92 | 2.47 |
| 14:45 | 3932 | Lion City Sailors vs Geylang Int. | 1.43 | 4.83 | 4.93 |
| 14:45 | 5149 | Albirex Niigata (SIN) vs Hougang United | 1.29 | 5.55 | 6.58 |
| 15:00 | 2954 | Akhmat Grozny vs FC Krasnodar | 2.36 | 3.21 | 2.74 |
| 15:00 | 5296 | Uthai Thani FC vs Rajpracha FC | 1.62 | 3.22 | 5.52 |
| 15:00 | 5652 | ASK Bravo vs Maribor | 3.80 | 3.39 | 1.81 |
| 16:30 | 1625 | Uthongathi vs Cape Town All Stars | 2.56 | 2.71 | 2.86 |
| 16:30 | 3680 | Latina vs Potenza SC | 2.23 | 2.93 | 3.56 |
| 16:30 | 4065 | Pretoria Callies vs Tshakhuma Tsha Madzivhandila | 1.59 | 3.15 | 5.20 |
| 16:30 | 4173 | Viterbo Calcio vs Taranto Sport | 2.27 | 2.87 | 3.56 |
| 16:30 | 5122 | Polokwane City vs Casric Stars FC | 1.97 | 2.85 | 3.55 |
| 16:30 | 5967 | Venda Football Academy vs JDR Stars | 2.56 | 2.68 | 2.89 |
| 17:00 | 1882 | Domzale vs NK Radomlje | 1.68 | 3.39 | 4.52 |
| 17:00 | 2007 | Uzbekistan vs South Korea U20 | 2.65 | 2.91 | 2.65 |
| 17:00 | 4856 | FK Sumgayit vs Karabakh | 9.32 | 4.97 | 1.26 |
| 17:30 | 1046 | Kryliya Sovetov vs CSKA Moscow | 2.69 | 3.26 | 2.38 |
| 18:30 | 1695 | ISA Town vs Al Ittifaq Bhr | 2.32 | 3.16 | 2.84 |
| 18:30 | 2998 | Al-Tadamun Buri vs Malkiya Club | 7.25 | 4.56 | 1.35 |
| 18:30 | 4865 | Al Shabbab vs East Riffa | 1.94 | 3.00 | 3.99 |
| 18:30 | 5260 | AL Khalidiyah vs Sitra Club | 1.51 | 3.45 | 5.40 |
| 19:00 | 5506 | Istra vs Dinamo Zagreb | 5.76 | 3.96 | 1.46 |
| 19:30 | 4823 | NK Celje vs Olimpija Ljubljana | 2.67 | 3.08 | 2.43 |
| 20:00 | 1208 | AS Trencin vs Spartak Trnava | 3.25 | 3.15 | 1.94 |
| 20:00 | 1282 | Basaksehir vs KAA Gent | 2.11 | 3.18 | 3.43 |
| 20:00 | 1299 | Zenit St Petersburg vs Dinamo Moscow | 1.36 | 4.67 | 6.64 |
| 20:00 | 2129 | Pro Vercelli vs Juventus U23 | 2.66 | 2.94 | 2.83 |
| 20:00 | 2187 | Pro Patria vs Novara | 2.58 | 2.88 | 2.99 |
| 20:00 | 3808 | Calcio Lecco vs Feralpisalo | 2.82 | 2.82 | 2.77 |
| 21:00 | 2018 | VfB Oldenburg vs Borussia Dortmund II | 3.02 | 3.28 | 2.25 |
| 21:00 | 3067 | Waldhof Mannheim vs Ingolstadt | 1.96 | 3.49 | 3.54 |
| 21:00 | 3412 | Saarbrucken vs Bayreuth | 1.54 | 4.18 | 5.18 |
| 21:00 | 5496 | Dynamo Dresden vs Duisburg | 1.73 | 3.61 | 4.46 |
| 21:00 | 5636 | Freiburg II vs Wehen | 2.51 | 3.32 | 2.63 |
| 22:00 | 1720 | Tottenham W vs Leicester City FC W | 1.61 | 3.64 | 4.89 |
| 22:30 | 1117 | Brighton vs Crystal Palace | 1.43 | 4.20 | 6.59 |
| 22:30 | 1724 | Southampton vs Brentford | 2.84 | 3.19 | 2.36 |
| 22:45 | 2238 | Blackburn vs Reading | 1.76 | 3.40 | 4.40 |
| 22:45 | 2571 | Luton Town vs Bristol City | 1.80 | 3.39 | 4.19 |
| 22:45 | 2766 | Hull City vs Burnley | 4.32 | 3.31 | 1.80 |
| 22:45 | 3950 | Huddersfield vs Norwich City | 4.09 | 3.44 | 1.80 |
| 22:45 | 5687 | Tiverton Town vs Hayes Yeading United | 2.69 | 3.72 | 2.18 |
| 22:45 | 5761 | Cardiff vs West Bromwich | 3.09 | 3.09 | 2.26 |
| 22:45 | 5926 | Swindon Supermarine vs Gosport Borough | 1.62 | 3.95 | 4.36 |
| 23:00 | 1364 | Virtus Francavilla vs Juve Stabia | 2.32 | 3.08 | 3.19 |
| 23:00 | 1897 | Foggia vs Monopoli | 1.80 | 3.14 | 5.11 |
| 23:00 | 2925 | Real Madrid vs Liverpool | 2.34 | 3.52 | 2.65 |
| 23:00 | 4056 | Sunderland vs Sheffield Utd | 3.00 | 3.20 | 2.25 |
| 23:00 | 5467 | Napoli vs Eintracht Frankfurt | 1.51 | 4.03 | 5.62 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Machi 15, 2023

Nipashe



UKURASA 22

## Guardiola aipa ubingwa Arsenal EPL

# SIMBA WAUNGANA KUIUA HOROYA AC



Kibu

●●●Yasema sasa ni nguvu moja kwa Mkapa Jumamosi, Kibu naye arejesha majeshi...

**Na Saada Akida**

ZIKIWA zimebaki siku mbili, Alhamisi na Ijumaa kabla ya Jumamosi kushuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Horoya AC ya Guinea kwenye mechi yao ya tano ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uongozi wa klabu hiyo umesema umemaliza makundi yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi na sasa wamekuwa kitu kimoja kuelekea mchezo huo unaoweza kuamua hatima yao ya kutinga robo fainali.

Simba inahitaji ushindi katika mchezo huo ili kuungana na Raja Casablanca ya Morocco katika Kundi C kutinga robo fainali ya michuano hiyo, na endapo itapoteza ama kutoka sare, itajiweka katika wakati mgumu kwani itategemea hesabu za vidole kulingana na matokeo ya mechi za mwisho.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again', amesema licha ya kuwapo kwa mapungufu katika kikosi chao, mashabiki wanatakiwa kuungana na kuisapoti timu yao katika mchezo huo utakaopigwa majira saa moja usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Try Again, alisema kulingana na kibarua kigumu cha mechi hiyo iliyopo mbele, viongozi na wachezaji pamoja na wanachama wote hawana budi kuwa wamoja ili kuongeza nguvu kuweza kushinda dhidi ya Horoya AC.

Alisema viongozi wamefanikiwa kuondoa makundi yaliyopo na sasa wanachama na Wanasimba wote ni wamoja na kurejesha ile kaulimbiu yao ya "Simba Nguvu Moja".

"Wanachama kwa sasa ni muda wa kushikamana kufanikisha malengo yaliyopo mbele yetu ya kucheza robo fainali, suala la maboresho ya kikosi ni hapo baadaye. Kwa sasa Wanasimba wote tunatakiwa kuwasapoti hawa wachezaji waliyoifikisha Simba katika nafasi ya tisa katika viwango vya Shirikisho la Soka Afrika kwa ngazi ya klabu.

"Hao ndio wameifanya Simba kuwapo hapo licha ya kuwapo na maingizo mapya akiwamo Mosses Phiri, Jean Baleke ambaye katika michezo michache aliyocheza amefunga mabao manne kwenye ligi, bado tunahitaji kuwapa muda nyota wetu wapya," alisema Try Again.

Aidha, alisema Simba imekidhi vigezo vya kucheza Kombe la Super League kupitia wachezaji hao waliopo sasa, licha ya kwamba wapo wanaoamini kikosi chao kina madhaifu na kutakiwa kukiboresha.

Mwenyekiti huyo alisema malengo yao ni kufanikisha kucheza michuano hiyo ya Super League kwa kufanya vizuri ili Simba ishike nafasi ya tano kwenye viwango vya CAF.

"Malengo yetu tukimaliza Super League, tutakuwa 'Top Five' (tabo bora), ninaimani kufika huko tutakuwa makini, viongozi tuko makini tunafanya kazi bila kulala wala kuchoka," alisema na kuongeza:

"Sisi ni viongozi na si wapenzi, tunatakiwa kufanya majukumu yetu kiuweledi mkubwa, kuhusu usajili na mapungufu ya kikosi tunayaona na tutayafanyia kazi," alisema Try Again.

Katika hatua nyingine, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kiungo mshambuliaji wao, Denis Kibu, amerejea na yupo fiti kwa ajili ya mchezo huo.

## Yanga yaiandalia dozi kali Monastir

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikihitaji pointi tatu tu ili kufuzu hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika itakaposhuka Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii, imetambua kuwa inahitaji kuwa fiti zaidi kwa dakika zote 90 ili kuwakimbiza mchakachaka US Monastir ya Tunisia, hivyo kwa sasa inapiga mazoezi mara mbili kwa siku ikianzia gym hadi uwanjani.

Jana asubuhi Yanga ilifanya mazoezi ya gym Gymkhana, Dar es Salaam kwa saa mbili na jioni walifanya ya uwanjani katika kambi yao ya Avic Town, Kigamboni kwa saa mbili chini ya Kocha wa Viungo, Helma Gueldich.

Mazoezi hayo yameelezwa ni kwa ajili ya kutafuta stamina na yalihudhuriwa na wachezaji wote huku kiungo Bernard Morrison aliyekuwa majeruhi akiwa sehemu ya maandalizi ya mchezo huo wa hatua ya makundi wa Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema anafahamu vizuri mbinu za US Monastir na wanavyocheza, hivyo wamelazimika kuongeza muda wa mazoezi ikiwamo kwenda gym kutafuta stamina.

Alisema mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wanahitaji kusaka ushindi wa alama tatu ili kufanikiwa kucheza hatua ya robo fainali ya michuano

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042